# AGANO LA KALE

## KITABU KU MASOMO WA KWANZA YA INCHI YETU




**CENTRE DE LA MISSION ORTHODOKSE**
**KOLWEZI KONGO**
**2000**

**Watoto wepenzi,**

**Hii mafundisho mutasoma ndani ya kitabu hiki ilifanyiwa mbele ya kufika miaka mingi Bwana wetu Yesu Kristu, MwokoziI wa dunia. Inaitwa Agano la Kale. Na maana yake iko ile Masikilizano Mungu Alifanya pamoja na watu wa Izraeli. Ni kusema ni malako moja Mungu Aliwapatia watu, ya kama Atatuma Mwana wake wa Pekee juu ya kuokoa watu.**

# KIPINDI CHA KWANZA

## Hadisi (historia) ya Agano la Kale

## Hadisi mbele ya Patriarshi

# 1. - KUINGIA

Wakati tunasimama mbele ya nyumba moja mnene na ndefu tunashangaa na tunakumbuka ule aliyefanya hii kazi ya kawaida ….
Vilevile tunakumbuka wakati tunaona mafendo mengi na mazuri ya mtu.
Wakati tunaangalia radio moja, television moja, chombo moja ao kila kitu mtu anaweza kufanya, akili yetu inaenda kwa ule mtu aliyefanya, kwa sababu hakuna kitu kinaweza kujifanya chenyewe.

Tunashangaa mtu juu ya hii kitu kinene na kikubwa alifanya. Lakini, mara ngapi inafaa kushangaa vile viko pembeni yetu! Sawa kwa mfano: mbingu isiyo na mpaka, jua na miangaza yake mingi, mwezi anayengaa usiku na nyota isipo hesabika (kubalulika) inayoangaza mbingu nzima.

Tena inafaa kushangaa ile inchi tunayokaa, majani yake na maua ya rangi ya kuachana. Tunapashwa kushangaa nyama kali na isipo kali.
Inafaa kushangaa bahari na samaki iliyo ndani yake na nyama na majani ingine iliyo ndani yake.

Na mwisho inafaa kushangaa mtu aliye kiumbe cha kwanza kati ya viumbe vingine vyote ndani ya hii dunia.

Viumbe vyote Mungu aliviumba, Yeye mwengewe Mwenyezi, na akili kamili

## 2. - Mungu Aliumba vyote

Mbele ya miaka mingi, hii dunia, sisi tuko tunaona sasa, haikuwako. Hata mbingu na nyota yenyi mwangaza. Hata hii inchi na nyama yake. Hata majani yoyote pamoja na watu wote hawakuwako. Fasi yote ilikuwa pasipo kitu hata kimoja ila Mungu wa milele Yeye alikuwako.

Mungu, sawa vile Yeye eko Mwenyezi, Aliumba hii dunia nzuri sisi tukotunaona pembeni yetu. Na tena aliumba na ingine dunia ile sisi hatuione na macho ya mwili wetu. Hii iko dunia ya roho. Ni kusema dunia ya Malaika wanaotulinda ku kila kitu kibaya.
Hii yote Mungu aliumba na hekima mingi mpaka na neno lake muda wa siku sita. Ni kusema kwa wakati mrefu wa siku sita.

Mwanzo, Mungu aliumba mbingu na dunia sawa vile Biblia Takatifu inatwaambia. Ile wakati dunia ilikuwa haijatengenezwa. Ilikuwa jangwa (desert) na tupu. Giza ilikuwa ikifunika vilindi. Hata hakukuwa kitu chenyi uzima.

Ile siku ya kwanza Mungu Alisema:
Mwangaza uwe na mara moja mwangaza ulifanyika. Ile wakati Mungu aliachanisha mwangaza na giza. Na hii nuru aliita Mchana na hii giza aliita Usiku.

Ile siku ya pili Mungu alisema: Mbingu na inchi ifanyike na ilifanyika.

Ile siku ya tatu Mungu alitosha maji ya inchi. Vile iliachanishwa bahari na inchi. Kisha Mungu Alisema miti na majani ya kuachana iote inchini. Basi ni hivi inchi ilifanyiwa na majani mengi ya rangi ya kijani (verte). Fasi yote iliota miti na chemchemu, mitoni na visanga vilionekana.

Ile siku ya inne Mungu alisema ile nyota kubwa mbili. Jua na Mwezi, ionekane mbinguni na nyota ingine isipo kuhesabika (kubalula).
Hii yote inaangaza inchi na inaachanisha Mchana na Usiku. Jua inaangaza Mchana, Mwezi na Nyota inaangaza Usiku.

Ile siku ya tano Mungu alisema, nyama ya bahari na ndege ya mbinguni ya kuachana iliumbwa.

Ile siku ya sita Mungu alisema nyama ya pori iumbwe iliumbwa.

**MAULIZO**

1. - Namna gani inaonekana nguvu, Uwenyezi wa Mungu?
2. - Aliumba nini ya kwanza na kisha ya kila siku?

## 3. - Mungu Anaumba mtu

Mungu aliona yote aliyeumba. Ni kusema: mbingu na nyota; inchi pamoja na majani na nyama yoyote. Hii yote ilionekana kuwa nzuri sana. Na ya hii mambo Mungu alisikia furaha sana.

Lakini kati ya hivi viumbe vyote hakukuwe kile kiumbe kilichoweza kuongoza hivi viumbe vyote. Ni hivi Mungu alikamata mpango wa kuumba mtu, mtoto wake mpendwa.

Basi alikamata udongo na alifanya mtu. Kisha aliipulizia kwa uso wake Pumzi yake Takatifu akimpatia hivi Uzima na nafsi ya milele.

Alimpatia akili na neno. Alimpatia nguvu juu ya kusikia na kuwaza. Vile Mungu aliumba ule mtu wa kwanza wa vitu viwili.

Alimupa mwili na nafsi na alimuita Adamu maana yake: Aliyetoka ku odongo. Huyu eko kiumbe kamili kabisa cha Mungu mbele ya viumbe vyote. Sawa vile Mungu hakupende Adamu kuishi peke yake, aliwaza kumpatia msaidizi wake. Basi Alibeba ubavu moja wa mwili wa Adamu aliumba mwanamke, msaidizi wa uzima wake. Na huyu mwanamke alimuita Eva, maana yake: Uzima. Ni hivi iliumbwa jamaa ya kwanza ya hawa watu wawili.

Kiisha Mungu alibarikia watu hawa wa kwanza juu ya kuzaa watoto na kuishi sawa wakubwa wa hii dunia.

Kwa baraka ya Mungu hawa watu mpaka sasa wanafanya nguvu kuishi vizuri.

Ile siku ya saba wakati Mungu aliona ya kuwa viumbe vyake vyote vilikuwa vizuri sana alipumzika. Juu ya hii mambo siku ile iliitwa Sabato, ni kusema Siku ya mapumuziko. Mwisho, hii siku ilipianwa na siku ya Mu Juma (DIMANCHE) iliyo siku ya Ufufuo wa Bwana YEsu Kristu.

**MAULIZO**

1. - Ni nani eko kiumbe kamili cha Mungu? Na juu ya nini?
2. - Watu wa kwanza ni wanani? Na juu ya nini wanaitwa hivi?
3. - Siku gani ya Juma (semaine) tunapashwa kupumzika? Na juu ya nini?

## 4. - Paradizo

Mungu alipenda Adamu na Eva kupita viumbe vyote vingine. Ya hii mambo aliwapatia chakula ingine na nyumba ingine. Basi Mungu mwema kamili aliwaweka hawa watu wa kwanza kukaa ndani ya Paradizo. Hii Paradizo ilikuwa shamba moja mnene na nzuri kabisa. Katikati yake ilipita mitoni Tigri na Efrati, ile fasi ya Mashariki kuko inchi inayoitwa Mesopotamia. Ndani ya hii shamba wazazi wetu wa kwanza waliishi kimya na nyama ndogo na nene. Ndege ya rangi mbalimbali iliruka fasi zote na sauti zao lilileta furaha kubwa ku watu hawa wa kwanza. Miti mingi ya kuachana iliwapatia matunda mengi. Majani ya rangi ya kuachana na maua (fleurs) ilitawanyisha (kusambalisha) manukato yao fasi zote.
Hii mitoni mnene na mdogo ilipita katikati ya hii shamba ililet maji yao ku miti na ku majani.
Mu hii fasi ya ajabu waliishi watu wa kwanza na furaha tele.
Hakuna kitu hata kimoja kiliweza kuwakosea. Vitu vyote sawa nyama na miti vilikuwa mikononi mwao.

Wakati Mungu aliweka watu wa kwanza ndani ya Paradizo alisema kwa Adamu hivi: "munaweza kula matunda yote iko ndani ya Raradizo lakini musile matunda ya hii mti inayoitwa "Mti wa ugahamu wa vitu vizuri vibaya". Mungu aliwapatia hii amri juu ya kuwapima kama watamutii.
Tena aliwaambia : "Kama hamunisikie, mukila matunda ya hii mti itamifikia mateso mengi. Mara moja mutatoka inje ya Paradizo, mutapoteza hii furaha yote mukona yo sasa, na mwisho mutakufa Mungu mwema aliwapatia hii amri na aliwaacha kuishi katika Uhuru ndani ya Paradizo.

**ULIZO**
1. - Paradizo ilikuwa nini na namna gani kule watu wa kwanza waliishi?

## 5. - Watu wa kwanza wanakataa kutii na Mungu Aliwatosha mu Paradizo

Watu wa kwanza ndani ya Paradizo walikuwa wanapata vitu vyote vizuri bila mchoko. Waliishi mule bila sikitiko, walilima udongo, na walipata furaha ya kila namna. Sawa vile walichunga amri ya Mungu walikuwa na furaha.

Lakini ile uzima wao wa kimya na furaha ulisimama.
Shetani alitamani furaha yao na aliweka ndani ya akili yake namna gani aliweza kuwaambia kukataa hile amri ya Mungu Baba yao.

Siku moja Eva alikuwa akijitembeza mu Shamba, akaona Shetani aliyejigeuza nyoka. Wakati alikaribia karibu yake, huyu nyoka alimuuliza na mafaa ya uongo mu namna hii :
- Eva ni kweli Mungu anamikataza kula matunda yote iko ndani ya Paradizo?

Eva alijibu:
- Hapana, tunaweza kula matunda yote iko ndani ya Paradizo, lakini mpaka ile matunda ya ule mti wa katikati ya Shamba letu, tunakatazwa kula. Kama tunakula hii matunda, Mungu alitwaambia ya kama tutakufa.

Lakini Nyoka alisema:
- Lakini kama munakula matunda ya hii mti itamipatia akili mingi.

Na hamuwezi kufa, lakini mutakuwa sawa Yeye. Ni kusema na mweye mutakuwa wa mungu.

Eva alisadiki ile sauti ya uongo ya Shetani. Aliangalia na mafaa matunda ya hile mti. Alinyangua na kufungua mkono wake, akakata tunda moja na akaikula. Kiisha alimpatiako mume wake, naye akala.

Tangu ile wakati walikula hii tunda walisikia ya kama walifanya kosa nene. Sikitiko na uzito mingi iliingia ku roho yao. Na wakati usiku ulifika, walisikia woga sana. Namna gani sasa wataangalia Mungu?

Kiisha muda kidogo walisikia shindo ya Mungu aliyekuwa akitembea ndani ya Paradizo sawa vile alikuwa anafanya kila siku.

Wakati Adamu na Eva walimusikia, hawakwende kumupokelea, sawa desturi yao ya zamani kwa sababu walisikia haya na walifichama ndani ya pori.

Mungu alimuuliza Adamu:

- Mtoto wangu Adamu, uko wapi?

Kwa mtetemeko mkubwa Adamu alijibu:

- Bwana, nilisikia sauti yako na nilifichama.

Mungu alimuuliza tena :

- Juu ya nini uliogopa? Ulikula tunda ile nilikufunga kula ?

Adamu aligombana sana juu ya kusema ya kama haikuwa kosa lake.

Ni hivi alisema:

- Mimi sikukosa hapana, mpaka huyu mwanamke Wewe ulinipatia njo aliniletea na mimi nikala.
- Mungu alimuuliza Eva;
- Ulikula tunda ile Miye nilimikataza kula?

Eva alijibu kwa woga mingi:

- Bwana, nyoka aliniogofya na nikala.

Mungu alisikitika mingi kwa sababu Adamu na Eva hawakumtii. Basi akawaambia ya kama hawawezi tena kuishi ndani ya Paradizo.

Inapashwa kutoka inje kutumika nguvu kazi ya mashamba na watapata chakula chao kwa jasho mingi. Na Eva atazaa watoto wake kwa uchungu mingi.

Kisha wakati kidogo walikuwa inje ya Paradizo. Walisikia ya kama walipotesha ile uzima wao na furaha kwani walikanyanga Amri ya Mungu.

Kila wakati walikumbuka ile uzima wao ndani ya Paradizo, walitosha machozi mengi.

Lakini Mungu Mwema kamili na mwenyi haki hakuacha kupenda viumbe vyake. Kweli aliwaapiza kwa sababu ilipashwa kufanya vile na aliwatosha ndani ya Paradizo. Lakini Yeye hapana kuwaacha bila kuwachunga. Tangu ile wakati wa kwanza alitengeneza namna ya kuwapa wokovu wao. Aliponyesha umivu yao na ile malako aliwapatia ya kama atatuma Bwana Yesu Kristu ule atakuwa Mwokozi wa dunia.

Hii malako Mungu aliwapatia watu wa kwanza inaitwa Evangelio ya kwanza. Hii malako yake inaonekana kuwa mapendo yake makubwa aliyeonyesha mbele ya watu wote.

Adamu na Eva walianza kuendelesha uzima wao katika mateso na sikitiko mingi na ile kitumaini ya kama Mungu atawasaidia.

**MAULIZO**

1. - Watu wa kwanza waligeuka wa Mungu wakati walikula ile tunda?
2. - Namna gani Shetani alilanda watu wa kwanza?
3. - Ile Evangelio ya kwanza ni nini? Na iko na faida gani kwetu sisi?

## 6. - Kujaa maji kwa dunia nzima.

Adamu na Eva walizaa watoto wengi, wanaume na wanawake. Hawa watoto nao walizaa wengine na hawa wengine nao vilevile walizaa wengine na vile watu walikuwa wengi duniani.

Lakini wale wote hawakuchunge imani kweli mbele ya Mungu. Kipande kweli kinene cha watu kilikataa kutimiza mapenzi ya Mungu. Katikati yao ilitawala majivuno na kazi mbaya.
Mungu alisikitika sana juu ya hii uharibisho wa watu. Lakini nao walifanya kazi mbaya kupita kazi ingine mbaya. Basi Mungu alikamata mpango wa kuharibisha watu wote juu ya kugeuza akili na uzima wao.

Katikati yao kulikuwa mtu moja wa heshima mbele ya Mungu na mwenyi haki na jina lake ilikuwa Noa ao Noe.
Yeye alikuwa na watoto watatu waliekuwa wanaisha kuoa:
Semu, Kamu na Yafeti. Huyu Noa pamoja na jamaa lake Mungu hakupenda kuwaharibisha kwa sababu yeye alikuwa mtu mzuri. Ni hivi Mungu alitaka na yeye aendeleshe uzima wa watu wa dunia.

Kiisha Mungu alimwambia Noa atengeneze Safina (bateau) mnene. Hiyo wakati alikuwa anatengeneza Safina watu wengine walikuwa wakiendelesha kuishi bila kufanya kitubio na kufanya zambi ya kuachana.
Noa alifanya vile Mungu alimwambia. Aliingia ndani ya Safina na alibeba pamoja naye chakula na viumbe vyote mbalimbali. Kiisha kunigia kwao ndani, mvua ilianza kunyesha ya mingi siku na usiku muda wa siku makumi inne.
Maji ilipanda kabisa juu ya milima yote na inchi yote ya dunia.

Hata kiumbe kimoja hakikuokolewa. Kisha ile maji ilijaa dunia nzima mpaka Noa na jamaa lake na nyama ile iliingia na sauti la Mungu ndani ya Safina.
Ku mwisho mvua ilikatika na jua ilitoka mbinguni. Maji ilianza kushuka kidogo kidogo chini na ile Safina ilibakia juu ya chongo ya mlima Ararati mwenyi kuwa mu inchi ya Armenia.

Noa alisikia ya kama maji ilishuka na alituma ndege moja anayeitwa Kunguru (corbeau) juu ya kuangalia kama atarudia. Lakini yeye hakurudie. Akatuma kwa mara ya pili njiwa moja (pigeon) na yeye alirudia na jani la mzabibu (olivier) kinywani mwake.
Kisha Noa alifungua Safina na alitoka inje na jamaa lake na viumbe vyote vilivyokuwa karibu yake. Mara moja, juu ya shukrani yake mbele ya Mungu, alijenga fasi moja ya sadaka na alimshukuru Mungu ya ile wokovu wake. Mungu alipokelea sadaka yake na alimbarikia.

Maana ya hii Safina ni Kenisa ya Bwana Yesu Kristu. Na watu wale weko wazuri na wanaoishi karibu ya Kristu wao wataokolewa kwa uharibifu wa zambi.

## 7. - Mnara wa Babeli.

Wale watu walizaliwa na Noa waligeuka wengi kisha wakati kidogo. Ile wakati wa kwanza walibakia pamoja. Walikuwa na mawazo ya pamoja na walisema lugha mpaka moja tu. Lakini sawa vile fasi hii ya kukaa ilikuwa kidogo, uzima wao ulikuwa nguvu. Kwa hivi walikamata mipango ya kuachana juu ya kuishi vizuri kupita.

Mbele ya kwenda fasi mbalimbali, walikamata mipango juu ya kujenga mnara moja mrefu. Walizania ya kama vizazi vya wale watu watakaozaliwa, wakati wataangalia hii mnara, watastajabu wale watu waliojenga. Na hivi walianza kuijenga. Waliwaza ya kama wako na nguvu sawa Mungu. Na waliwaza ya kama ule mnara wao utafika mpaka mbinguni. Majivuno yao inaisha kupita. Halafu Mungu alikamata mipango ya kuwaapiza juu ya hii kazi na mawazo yao. Majivuno iko kitu kibaya kabisa.

Basi Mungu alileta mambo moja isiposikilika kwa lugha ya watu wote. Kila mtu alisema mu lugha yake kwa ndugu yake lakini huyu yeye alisikia mambo ingine. Hawakuweze kuendelesha kazi yao ni hivi waliacha kazi yao mu katikati. Ile mnara inaitwa: “Mnara wa Babila” iko bila kusikilizana kwa watu kati yao.

Kiisha hii mambo watu wote walitawanyika fasi zote ya kuachana. Ni hivi kulizaliwa kisha mataifa mengine yenyi lugha yao na namna ya maisha yao ya kuachana.

Mu hii wakati watu walisahau Mungu mara ingine. Walianza kuabudu kila kitu cha dunia kilicho wapendeza, nikusema Jua, Mwezi, Nyota na Mitoni. Tena waliabudu nyama sawa Mungu. Vilevile walianza kusadiki kwa wa mungu wengi. Juu ya wale wa mungu wa wongo walifanya sanamu ya mbao ao ya maibwe. Hii sanamu ya majibwe ao ya mbao waliita mu francais “Idoles” na waabudu sanamu ‘Idololatres”.

Lakini Mungu wetu Mpenda wanadamu hakuacha mtu mu hii hali. Aliwatumia watu wenyi mwangaza juu ya kuwafundisha mapenzi yake.

**MAULIZO**

1. - Juu ya nini Mungu alileta mambo ya kusumbulia mu ma lugha isipokusikilika ku wale watu waliotaka kujenga Mnara wa Babila? Ni kusema mtu moja hapana sikia mwengine anayosema.
2. - Ile hadisi (historia) ya Mnara wa Babila inatufundisha nini?




# KIPINDI CHA PILI

## Wapatriarchi Wakubwa

### 1. - Matangulizi

Wapatriarishi walikuwa wakubwa wa majamaa. Na kila mmoja wao alikomea na alikuwa mkubwa wa kabila mnene. Hawa walikuwa watu wakuchunga nyama na waliishi mu pori. Mara mingi walibadirisha fasi yao ya kukaa juu ya kupata chakula cha wanyama wao. Walikuwa watu wazuri na walimuheshimia Mungu. Wale watu Mungu aliwaachanisha juu ya kupatia watu wake wokovu.

Mungu mwenyewe mpenda wanadamu tangu ile wakati alifukuza watu wa kwanza mu Paradizo, aliwapatia malako yake ya wokovu wao. Ile malako yake aliikumbusha kila wakati kwa Wapatriarshi wao. Moja kati yao alikuwa Abrahamu.

## 2. - ABRAHAMU

Abrahamu aliishi mu mji moja wa Mesopotamia ulioitwa Harrana. Alikuwa mtu mzuri na wa heshima mingi mbele ya Mungu. Alimuabudu Mungu katika ukweli na alitii mapenzi yake Mungu.

Mungu aliyependa watu alimufikia siku moja Afrahamu na akamwambia:
"Ee Abrahamu, ile fasi unakaa inajaa watu wasipo imani na heshima mbele yangu. Basi acha hii fasi na kuja kuishi mu ile fasi Miye nitakuonyesha. Kule, mimi nitaongeza watu wa kizazi chako sawa mchanga. Kwa ajili yako watabarikiwa makabile yote ya dunia".

Abrahamu alipaswa kuacha inchi yake na jerani yake juu ya kwenda ku fasi moja yasipo kufahamia, bila njia na namna ya kuweza kutembea. Kiisha hatari kule ilikuwa mingi. Karibu yake alibeba bibi yake Sara, mwipwa wake Loti aliyempenda sana, kwa sababu hasikukuwe na watoto. Fasi zote Mungu alimuonyesha alitembea na mali yake yote. Kisha siku mingi, wakati alitambuka mtoni Yordani, alifika ku fasi moja nzuri yenyi miti mingi jina lake iliitwa Kanaana. Watu wa Kanaana walimpatia Abrahamu jina la Ivri kwa sababu alivuka mtoni Yordani ni kusema ule mtu anavuka. Tangu hiyo siku kabila la Abrahamu ilibeba jina la Ebrania.

Ile inchi ilikuwa ile Mungu alimlaka Abrahamu mwenyewe aliyemtukuza Mungu.

Mungu alifurahi kwani Abrahamu alifuata Sauti yake. Mbele alifika kwake mara moja mu mfano wa Malaika watatu. Abrahamu aliwapatia chakula mu nyumba yake. Hii wakati alimbarikia na alimwambia:

- Abrahamu mimi nitakufanya kuwa Patriarchi, ni kusema Mkubwa wa taifa moja itakaokaa pa hii fasi. Ya watu wa kabila lako atazaliwa Mwokozi wa dunia.

  Abrahamu na Sara bibi yake, kwa baraka ya Mungu, waliishi katika amani na haki. Walitimiza mapenzi Yake, walikuwa watu walioheshimu Mungu na walipenda ndugu zao. Walipata mali mingi na watu wengine waliwapenda na waliwaheshimu. Kwa hii mambo walitukuza Mungu juu ya vitu vyake yvote vizuri aliwapatia.

  Lakini walizeeka bado kuzaa mtoto hata moja. Juu ya hii, walikuwa na sikitiko mingi. Japo hiyo walichunga kitumaini chao kwa Mungu na walianza kumuomba awasaidie wazae.

  Walisakidi ya kama Mungu atatimiza malako yake ya kuwa. Atazaliwa mtu moja wa kabila la Abrahamu na Yeye atakuwa Mwokozi wa dunia.

  Ni kweli, kisha sala zao mingi, Mungu aliwastahilisha kuzaa mtoto moja mu jina lake Isaaka.

  Isaaka alikuwa mtoto moja mzuri sana na alifanya utii mbele ya wazazi wake. Katika mapendo mingi walimuona mtoto weo huyu kukomea.

  Sawa vile Mungu alitaka kupima imani na utii ya Abrahamu. Alifika kwake siku moja na alimwambia kubeba mtoto wake wa pekee Isaaka na kupanda kilima kimoja. Na kule alipaswa kumtolea mtoto wake sawa sadaka kwake Mungu.

  Abrahamu alisikia kwa unyenyekevu hii amri ya Mungu na roho yake ailipasuka na sikitiko. Kiisha alitosha sikitiko yake wakati aliwaza ya kama ilikuwa mapenzi ya Mungu na kama alipaswa kuitimiza. Basi alibeba mtoto wake Isaaka na alienda ku ile fasi ya sadaka. Njiani Isaaka aliuliza baba yake:

-Baba, kondoo ile tutafanya sadaka kwa Mungu iko wapi?

Hii maneno ya mtoto ilileta huzuni ku roho ya Abrahamu na alijibu hivi:

- Mtoto wangu, Mungu atatengeneza hii mambo.

Wakati walifika ku ile fasi Abrahamu alikamata mtoto wake na alibarikia hii fasi ya sadaka. Wakati alikuwa tayari ya kuuwa mtoto wake, Malaika wa Mungu alikamata mukono na kisu chake na alimwambia:

Abrahamu, Mungu anaona imani yako na utii wako. Kwa mapenzi yake usiuwe mtoto wako lakini uwa kondoo mwanaume huyu eko hapa karibu. Wakati alitezama, Abrahamu aliona kule karibu kondoo moja aliyekuwa tayari kwa kutolewa sadaka.

Isaaka alivekuwa mwenyi kosa na aliyekwenda ku hii fasi ya sadaka anafanana na Bwana Yesu Kristu aliyetoa mwili wake kama sadaka juu ya wokovu wetu.

Kisha Abrahamu alimshukuru Mungu. Mara ingine alianza kusikia sauti ya Mungu ikimuhakikisha ya kama ataongeza wale watu watakaobatizwa wa kabila lake, ya kama kwa ajili yake itabarikiwa mataifa yote ya dunia kwa maana alionyesha imani yake ya nguvu kwa Mungu na alisikia mapenzi yake. Vilevile Abrahamu mbele ya macho yetu eko mfano wa kweli wa imani na utii wa watu wote.

**ULIZO**

1. - Unaweza kuniambia na kuambia wengine hadisi (historia ) na imani nguvu ya Abrahamu?

## 3. - Ndoa ya Isaaka na Reveka

Wakati Isaaka alifika pa kipimo cha kuoa baba yake Abrahamu aliwaza ya kama ilipaswa kubeba bibi wa inchi yake, ni kusema wa mu Mesopotamia (Iraki).

Basi siku moja aliita mtumishi wake Elizeo akamwambia:

-Elizeo, kwenda ku fasi ya wababa wetu juu ya kutafuta bibi wa Isaaka. Beba karibu yako vitu vya kuachana juu ya kupatia jamaa la ule binti mzuri utapata kufuatana na baraka ya Mungu.

Elizeo, kisha safari ndefu ya mchoko mingi, alifika inje ya ule mji alikaa ndugu ya Abrahamu. Alisimama karibu ya kisima kimoja, pahali pale kila mangaribi watu na wabinti wa mgini walikuwa wanashota maji.

Mbele ya kupumzika, alifanya sala yake kwa Mungu:

- Mungu wangu, unionyeshe ule binti weye utataka akawe bibi wa Isaaka. Ule mwenyewe atakayenipatia maji ya kunywa miye na ngamia yangu, huyu atakuwa bibi wa Isaaka.

Alikuwa karibu ya kuisha sala yake wakati aliona ngambo ingine binti moja mzuri akija kwa kushota maji.

Elizeo alimuomba maji na huyu kwa haraka alimpatia maji na nyama yake. Basi, Elizeo alisikia ya kama huyu binti atakuwa bibi wa Isaaka. Ni hivi Elizeo alimuuliza:

- Baba yako ni nani? Na jina lako ni nani?

Huyu binti alimuonyesha wazazi wake ni wanani na ya kama jina lake ni Reveka.

Wakati alisikia hii yote Elizeo alimpatia vitu mingi. Huyu binti alienda mbio ku nyumba yao kuambia wazazi wake na ndugu yake.

Kisha huyu ndugu yake alienda kumuita Elizeo na alitayarisha chakula. Elizeo aliwaelezea juu ya nini alifanya hii safari kiisha aliomba wampatia Reveka juu ageuka kuwa bibi wa Isaaka.

Watu wote walisema: kweli, iko Mapenzi ya Mungu, Reveka atakuwa bibi wa Isaaka.

Ni kwa furaha kubwa walipokea hii sauti ya Elizeo. Kisha Reveka aliitika na Elizeo alileta kwao vya mingi vya kuachana.

Ni hivi mwisho wake Elizeo alibeba Reveka na kumpeleka ku Kanaana. Kule ilifanyika ndoa katika furaha mingi.

Isaaka na Reveka walikuwa watu wenyi heshima na imani mbele ya Mungu na waliishi na furaha mingi.

Abrahamu, kiisha ndoa ya mtoto wake, aliishi tena miaka nakumi tatu na tano. Alikuwa anawashauria namna ya kuchunga imani ya kweli mbele ya Mungu na kufuata mapenzi Yake. Alikufa mzee na furaha mingi kwa sababu alistahilishwa kuwa Mkubwa wa ile taifa la Izraeli iliyekuwa taifa pendelevu la Mungu.

Mungu, kisha lufu ya Abrahamu, alionekana kwa Isaaka. Alimbariki na alimuhakikisha ile malako alimpatia baba yake ya kama siku moja atazaliwa Mwokozi wa dunia toka kabila lake. Ni hivi Isaaka eko Mkubwa wa pili wa mababu wa Bwana Yesu Kristu.

ULIZO

1. - Elizeo alifanya sala juu ya kupata Reveka. Hii mambo inatufundisha nini?

## 4. Watoto wa Isaaka- Yakobo.

Isaaka na Reveka walizaa watoto wawili: Yakobo na Izau.

Yakobo alikuwa mtu mpole, mpenda amani na mwaminifu kwa Mungu.

Kwa hivi Mungu alionekana kwake mara mbili mu namna ya ajabu na alimuambia mara ingine ile malako aliyopatia mababu wake.

Wakati walipoenda Mesopotamia ao Iraki, wakati usiku ulifika, alipumzika katika jangwa moja. Alipolala usingizi aliona ndoto moja. Ni kusema aliona mungazi moja mrefu sana kutoka chini mpaka mbinguni. Na Malaika wa Mungu walipanda na kushuka na sauti moja ilisikilika:

-Usiogope kwa sababu Miye ni Mungu wa Abrahamu na Isaaka. Hii inchi unalala nitakupatia wewe na watu wa kabila lako. Kwa ajili yao itabarikiwa makabila ya dunia nzima. Mimi nitakuwa karibu yako, nitakuchunga fasi zote utaenda, nitakusaidia juu siku moja ukarudie mara ingine pa hii fasi.

Yakobo aliamka na mtetemeko mkubwa. Aliwaza ya kama Mungu eko anakaa pa hii fasi. Kwa hii mambo aliita hii fasi “Nyumba ya Mungu”. Kiisha alimuomba Baba nwenyi kuwa Mbinguni. Yeye aliyemuonyesha hii mapendo mingi. Kiisha wakati ingine alijenga mazabahu juu ya kuonyesha shukrani yake kwa Mungu.

Wakati Yakobo alianza kurudia, karibu na kufika mu inchi yake, ilifika giza, ni hivi alikaa kwa kupumzika.

Kwa ndoto yake aliona ya kama alimpiga mtu moja nguvu sana. Tena aliwaza ya kama mtu huyu alikuwa Mungu. Na ni kweli Mungu alipenda kuonekana mu hii hali.

Hii wakati Sauti ya Mungu ilisikilika ikisema:

- Tangu sasa utaitwa Izraeli, ni kusema nwenyi nguvu, kwa sababu ulionekana kuwa nguvu kwa imani yako na utakuwa na ulinzi wangu. Tangu ile wakati watu wa kabila ya Yakobo, wa Ebrania, wanaitwa wa Izraeli.

Yakobo kweli alionekana nguvu kwani, mu miaka yote aliishi mu inchi yake alibakia mpaka mu imani moja ya kweli mbele ya Mungu, ule mababu wake Abrahamu na Isaaka waliabudu.

Yakobo alipata mali mingi na alizaa watoto kumi na wawili.

Majina yao ni hii : Rubeni, Simoni, Levi, Dani, Neftalini, Gadi, Yudasi, Isakhari, Zavuloni, Siri, Yozefu na Beniamini.

Ya hii watoto ilizaliwa makabila kumi na mbili iliobeba majina yao.

Yakobo alikuwa na furaha kubwa kwa sababu alikuwa na jamaa mnene. Alisadiki Malako ya Mungu ya kama atafanyiwa kuwa mkubwa wa taifa la Izraeli na ya kama toka watu wa kabila lake atazaliwa Mwokozi wa dunia.

## 5. - Yosefu anaenda Misri

Yosefu alikuwa mtoto wa Yakobo. Alikuwa mpendwa kuliko watoto wake wengine. Tangu udogo wake yeye alionekana kuwa mtoto mwenyi akili na mpole. Aliheshimu wazazi

wake na watu wakubwa tena aliwapenda ndugu zake kweli. Baba yake juu ya kumuonyesha mapendo yake alimuuzia mpila moja mzuri. Lakini ndugu zake wakati waliona hii mapendo aliokuwa nayo baba yao kwa Yosefu, walianza kumusikilia wivu. Hii wivu wao ilikomea ndani ya roho zao, kabisa kabisa wakati Yosefu aliwaelezea ndoto yake ya pili.

Aliwaelezea ya kama: Sisi wote ndugu tulikuwa mu mashamba na tulifunga vifulushi ya ngano kwani tulianza kuvuna. Kifulushi changu kilisimama, lakini vifulushi vyenu vilianguka chini na vilisujudu kile changu.

Ndugu zake walikasirika na walimwambia hivi:

- Unawaza ya kama wewe utakuwa mkubwa na sisi tutapiga magoti kwa kukusujudu?
  Kwa ile ingine ndoto yake ingine Yosefu aliona ya kama Jua (baba yake) na Mwezi (mama yake) na Nyota (ndugu zake kumi na moja) walimsujudu.

Sasa ndugu zake walikasirika juu ya wivu wao mbele ya Yosefu na waliweka mawazo mabaya ndani ya akili yao.

Siku moja Yakobo alimtuma Yosefu kwenda kutafuta ndugu zake wale walikuwa wanachunga kondoo zao. Ndugu zake wakati walimuona mbali waliwaza kumfanyizia mambo mubaya.

Ku mwanzo walimkamata na kumtosha ile mpila yake mzuri aliokuwa akivaa na walimtupa ndani ya kisima cha kukauka. Hii mawazo ilitoka ya akili ya ndugu yake mkubwa Rubeni aliyetaka wasimuue. Lakini Yudasi alileta shauri la kumuuzisha sawa mtumwa kwa watu waliokuwa wanapita kwa kwenda Misri. Kisha hii mambo ndugu zake walipasua mpila wake na kuiweka damu. Na hivi waliituma kwa baba yao.

Walimuonyesha ya kama waliipata porini na wanawaza ya kama mara ingine nyama ya pori ilimuuwa na kumla.

Yakobo alisadiki maneno yao. Akalia sana mtoto wake aliyepotea. Lakini Mungu alimchunga sana Yosefu.

Hawa watu wafanya bihashara (trafic), walienda kuuzisha Yosefu kwa Petefri aliyekuwa mpishi wa bwana mfalme Faraonio wa Misri. Petefri alimpokea mbio mbio Yosefu na alimuweka kuwa mtumishi nyumbani mwake, ni kusema kutumika kila kazi yake. Ni kweli kila kazi ya nyumba iliendeka vizuri kabisa, lakini bibi wa Petefri, aliyekuwa mbaya sana alimusitaka kwa bwana yake ya kama alipenda kufanya zambi naye. Bwana yake alimusadikia ni hivi aliweka Yosefu mu buloko. Lakini Yosefu yeye hakupoteza kitumaini chake hapana. Alikuwa na kitumaini ya kama Mungu atamusaidia. Hii iko mfano wake mzuri. Kiisha juu ya hii tumaini, walimtosha mu buloko.

**MAULIZO**

1. - Nini ilikuwa ndoto ya Yosefu?
2. - Namna gani Yosefu alienda Misri?

## 6. - Yosefu ndani ya Buloko

Ile wakati Yosefu alikuwa ndani ya buloko ule zamu alimpenda sana. Mchungaji mkubwa alimuhamuru kuwa mkubwa wa wale wafungwa wa ndani ya buloko.

Yeye Yosefu alikuwa anawashauria, anawatuliza na kuwaomba watubu, aliwaomba kufanya mapenzi ya Mungu na kuishi ndani ya uzima pasipo kosa. Na watu walimkamata sawa rafiki na ndugu yao.

Ndani ya hii buloko kulikuwa watu wawili waliomukosea mfalme Faraoni. Yosefu aliwakaribia na aliwaonyesha mapendo yake. Aliwashauria na aliwatuliza.

Lakini siku moja asubui aliwaona kuwa katika sikitiko. Aliwauliza juu ya nini? Na wao walimwambia ya kama waliona ndoto moja. Yosefu aliwaambia ya kama kukonamna ya yeye kufafanua ndoto yao kwa nguvu ye Mungu.

Mtu wa kwanza, ule aliyemwanga vinyo waji ya mfalme Faraoni alisema hivi:

-Mimi niliona majani matatu ya ule mti unayotosha vinyo. Ilikomea mbio, ilitosha majani na ilizao matunda mengi. Nilibeba matunda ya kuenea, niliikamua, niliiweka ndani ya kopo moja, nilimpatia mflme Faraoni na yeye aliikunywa.

Yosefu alimjibu hivi:

-Ndoto yako rafiki yangu iko nzuri. Kisha hii siku tatu watakutosha ndani ya buloko na utarudia kwa kazi yako. Ninakuomba sana, wakati utatoka hapa unikumbuke na mimi kwa sababu niko katika uzulumu.

Kisha ilifika wakati wa mtu mwengine, huyu mkubwa wa tanuru aliyesema hivi:

Miye niliona ya kama nilikuwa na vitunga vitatu juu ya kichwa changu moja juu ya ingine. Kile cha juu kabisa kilikuwa na vyakula vitamuvya kuachana vya mfalme Faraoni, lakini ndege ilikuja pembeni na ilikula.

Yosefu alijibu:

- Ndugu yangu, ndoto ni mbaya kwa sababu kisha siku tatu watakutosha mu buloko na watakuuwa.

Mambo ilipita mpaka vile Yosefu alifafanua ndoto zao. Ule wa kwanza walimtosha na aliende ku kazi yake. Na ule wa pili walimuuwa.

Lakini huyu mtu wa kwanza alisahau kusaidia Yosefu. Japo hivyo Yosefu hakupoteza kitumaini chake. Alikuwa mpaka na kitumaini kwa Mungu ya kama siku moja atapata haki yake.

## 7. - Mungu anamtukuza Yosefu

Kisha miaka mbili mfalme Faraoni aliona ndoto mbili. Aliita watu wake wa akili wa inchi yake, lakini hata moja hakuweze kuifafanua. Juu ya hii mambo alikuwa na sikitiko mingi. Ule mkubwa katika ndoto, alimpa Faraoni vinyo, alimkumbuka Yosefu. Alifika mbele ya Faraoni na alimwambia ya kama mtu moja wa Ebrania aliye ndani ya buloko anayeitwa Yosefu anajua kufafanua ndoto kweli. Faraoni alileta amri ya kumtosha na kumpeleka mbele ya macho yake.

Ile wakati mfalme Faraoni alianza kumuonyesha ndoto yake, alimwambia hivi:

- Mimi niliona ngombe saba nzuri na nene wakitoka ku mtoni Nili ya Misri. Kiisha kidogo wengine saba wakonde na wabaya walitokea.

Wale wa mwisho walikula wa kwanza. Niliogopa na niliamka. Kisha, aliendelesha Faraoni ndoto yake; nilipata mara ingine usingizi. Nikalota ya kama pa hii fasi paliota majani ya ngano saba mazuri sana na masuke mengi ya ngano. Kisha kidogo kukaota ingine majani mabaya ya kukonda pasipo masuke. Na hii ilikula ile ya masuke mengi. Nikapata sikitiko, akasema Faraoni, kwani hata mtu moja hakuweza kunielezea maana yao. Weye unasema nini?

Yosefu, wakati alisikia hii ndoto yake, sawa vile alikuwa na mwanagaza wa Mungu, alimjibu hivi:

-Mfalme wangu, ndoto yako mbili ina maana moja. Ni kusema ile ngombe saba mnene na ile majani saba manene na masuke inatuonyesha ya kama inchi yako ya Misri itapata vyakula vingi muda wa miaka saba. Kwa hii ngombe ya kukonda na ngano ya mubaya inaonyesha ya kama kutakuwa njaa kubwa muka wa miaka saba. Kwa mawazo yangu, mfalme wangu, aliendelesha Yosefu, iko vizuri kutafuta mtu moja wa nguvu na wa kweli. Ule utaonyesha aonyeshe watu wa Misri kulipa ngano mu hii miaka saba ya mavuno mazuri kwa ginsi kusikakose chakula mu hii miaka saba ya njaa.

Faraoni alisifu sana mawazo ya Yosefu. Mara moja akamtosha ndani ya buloko na akawaza kumpatia ile kazi ya kukusanya ngano fasi mbali mbali.
Alimwambia hivi:

-Hakuna mtu mwengine kupita nguvu ya weye. Paka weye utafanya kazi hii. Tangu sasa utakuwa mkubwa wa inchi yangu kiisha mimi. Na mara moja alimuonyesha ku mataifa yote. Ni hivi Yosefu alikuwa sawa Ministre wa Ekonomia. Alitumika na akili na mapendo kwa watu wote. Alisaidia ile inchi ya mfalme. Kama mtu moja eko mzuri na mwenyi imani na heshima mbele ya Mungu atamlipa na atamusaidia.

## 8. - <u>Ndugu ya Yosefu walienda Misri</u>

Katika miaka ile ya furaha Yosefu alijenga nyumba ya kuchungia ngano mu fasi nyingi ya Misri. Kisha ilifika miaka ya mateso. Watu wote waliteswa sana mpaka wale waliokaa Misri hawakuteswe. Tena kule walifika watu wa inchi zingine juu ya kuuza ngano. Na pale Kanaani, pahali palipokaa Yakobo na watoto wake palikuwa njaa mingi. Tangazo juu ya ngano ya Misri ilifika kule.

Yakobo wakati alisikia hii habari alituma mara moja watoto wake na feza na nyama inayoitwa ngamia juu ya kuuza mbegu ya ngano. Alibakia mpaka na ule mtoto wake mdogo kabisa jina lake Beniamini.
Hawa watoto wake wengine walipofika Misri walitafuta ule mkubwa mchungaji wa vyakula bila kujua ya kama huyu mkubwa ndiye ndugu yao waliyouzisha. Walipofika mbele yake walipiga magoti sura chini vile ilivyokuwa zoezo lao. Kiisha walimuonyesha ukomo wa safari yao.

Yosefu aliwafahamu mara moja na alifurahi sana. Akakumbuka baba yake, mama yake na ile miaka yeye alikuwa mtoto. Alikumbuka pia ndoto yake aliyoona. Alikumbuka vilevile ile kazi mbaya walifanya ndugu zake na alijiuliza rohoni mwake kama wapo tena na ile roho mbaya sawa zamani. Ni hivi alipima kuwauliza hivi:

- Nyinyi muko wapelelezi (espiona), munafika hapa juu ya kufanya kazi mbaya? Muko na Baba na ndugu?
  Wao walimjibu:
- Ee bwana wetu, sisi tuko watu wazuri, lakini juu ya njaa tuko nayo tunafika mbele yako. Baba yetu angali anaishi lakini ni mzee sana. Sisi wote watoto tuko kumi na mbili. Moja alipotea, mwengine anabakia karibu ya baba na sisi kumi tuko mbele yako.

Yosefu aliwajibu:
- Mimi simisadiki.

Kiisha alileta amri ya kuwafunga ndani ya buloko. Kisha siku tatu Yosefu aliingia ndani ya buloko na mtu moja aliyejua lugha ya Kiebrania na aliwaambia:
- Munaweza kubeba ile mbegu ya ngano munataka na kurudia nyumbani kwenu lakini moja wenu atabakia ndani ya buloko mpaka pale mutaniletea ndugu yenu wa mwisho. Vile nitahakikisha ya kama munaniambia kweli.

Wakati walisikia sauti yake, ndugu wake wote walisema katikati yao :

-Mungu atatuapiza kwa ajili ya kile kitendo chetu kibaya mbele ya ndugu wetu Yosefu. Tulifanya kazi ya matata pasipo mapendo mbele yake. Kwa hivi sasa tunateseka na haki.

Yosefu aliposikia ile sauti ndugu zake walianza kusumbulia juu ya Beniamini hakupendezwa kuonekana tena kwao. Alichofa kidogo mbali na alilia machozi. Kisha aliwapatia ruhusa ya kurudia mu inchi yao pamoja na mbegu ya ngano na alikamata mpaka jina moja ya Simoni. Kisha aliweka feza (makuta) waliotaka kulipa ngano yao. Aliwapatia chakula kwa safari yao na vile walitoka.

Wakati wa usiku walipokuwa wakipumzika moja wao alipofungua mfuko wake moja aliona feza ndani. Wengine nao vile vile waliona feza ndani ya mifuko yao. Walishangaa sana hii mambo na hawakuweze kuifafanua.

Walipofika Kanaani, walimwambia mambo yote baba yao. Walimwambia ya kama inafaa siku ya kwenda Misri kubeba mdogo wao wa mwisho Beniamini.
Yakobo aliogopa sana hii mambo na aliwaambia:

-Nilipoteza mtoto wangu Yosefu, mweye munaacha tena mtoto wangu mwengine ndani ya buloko Simoni, sasa munaomba mubebe Beniamini? Hapana, hii mambo haitafanyika hata. Pale pale akaanza kulia juu ya hii mambo ya watoto wake wawili waliopotea.

**MAULIZO**

1. - Namna gani Yosefu analeta mateso kidogo kwa ndugu zake?
2. - Juu ya nini ndugu ya Yosefu hawakumfahamu tena pale Misri?

## 9. - Yosefu anajijulisha kwa ndugu zake

Kiisha wakati kidogo ngano iliisha nyumbani mwa Yakobo, ni hivi alituma mara ya pili watoto wake Misri. Lakini wao hawakuweza kwenda bila Beniamini. Ni katika huzuni rohoni mwake aliitika kumtuma.

Aliwapatia vitu vizuri juu ya kupatia mkubwa wa Misri na feza ya kulipa ile ngano waliobeba safari yao ya kwanza na ya pili. Aliwabarikia nao walienda.

Wakati walipofika Misri, walifika mbele ya Yosefu. Yeye aliwapokelea na mapendo mingi na aliwauliza juu ya baba yao. Wao walimjibu ya kama baba yao eko vizuri na alimtumia vitu.

Yosefu wakati alisikia haya maneno na vile alimuona Beniamini alisikia furaha mingi na alianza kutosha machozi yake. Kisha aliwaita nduku zake, aliwafanyizia karamu mkubwa na aliwaweka katika mustari wa kipimo chao. Ya hii mambo ndugu zake walishangaa. Kisha chakula Yosefu alimwambia msaidizi wake kujaza ngano mifuko yao na kuweka ndani feza yao yote na kuweka ndani ya mfuko ya Beniamini ile kopo yake nzuri ile yeye alikuwa ananywia maji.

Siku moja walitoka kwa kwenda kwao. Walikuwa katika furaha sana kwa sababu walianza kurudia kwa baba yao. Lakini hawajatoka inje ya mji waaskari wa Faraoni walifika kuwabamba na waliwaambia:

- Munaiba ile kopo nzuri ya mkubwa wetu!
  Ndugu yake walishangaa ! Walisikia sawa radi inapika vichwani mwao ! Na walisema:
- Sisi wezi? Hapana bwana ! Kama mtu moja kati yetu aliiba, inafaa kumuapiza.
  Walitafuta na walipata ile kopo ndani ya mfuko wa Beniamini !
  Huyu mtoto alishangaa, kwa sababu hasikujue kitu, namna gani ilifanyika hii mambo. Ndugu wengine walisikitika sana. Ma askari waliwapeleka mbele ya mkubwa wao.
- Kazi gani mbaya mweye mulifanya ? Yosefu aliwauliza.
- Bwana wetu, sisi tuko watumwa wako, fanya kile unataka, walimjibu kwa woga mingi.
- Hapana, aliwaambia Yosefu. Mpaka ule aliyebeba hii kopo yangu njo atabakia mtumwa wangu! Mweye mutarudia ku inchi yenu.
- -Mkubwa wetu, onyesha mapendo yako mbele ya baba yetu. Yeye atakufa juu ya sikitiko yake kama hasitaona kati yetu mtoto Beniamini, alimjibu Yuda na sikitiko mingi. Tena alimwambia: Mkubwa wangu, unikamate mimi pa fasi ya Beniamini na umuache yeye arudie.
- Yosefu hakuweza tena kufichama mbele yao ni vile aliwaambia na machozi mingi ku macho yake akasema;
- Miye niko ndugu yenu muliouzisha, lakini Mungu alinichunga. Hii saa, wote walisimama pasipo kusema sauti na woga mingi.

Aliwaambia tena:

- Msiogope ndugu zangu. Hii mambo ilifanyika katika mapenzi ya Mungu. Mimi ninamipenda sana na nitamisaidia. Na vile aliwapatia ndugu zake furaha na machozi mingi.

**MAULIZO**

1. - Namna gani Yosefu alisikia ya kama ndugu zake hawakuwe na mawazo mabaya rohoni mwao ?
2. - Namna gani munaona mfano wa Yosefu mbele ya ndugu yake?

## 10. - Yakobo anaenda Misri

Ndugu za Yosefu walirudia Kanaani kwa furaha mingi na waliambia baba yao ya kama walipata ndugu yao Yosefu. Eko mzima na eko mkubwa wa inchi ya Misri na anataka sisi wote twende kuishi kwake pamoja naye.

Yakobo, ya kwanza hakusadiki hii habari. Ilonekana kwake sawa ndoto. Lakini wakati aliona vile vitu alimtumia Yosefu, alisadiki na alikamata mipango juu ya kwenda Misri kuangalia mtoto wake mbele ya kufa. Kiisha alimshukuru Mungu na furaha mingi kwa sababu Alichunga watoto wake na kabisa Yosefu.

Yosefu wakati alisikia ya kama baba yake anafika, alienda inje ya mji kwa kumpokelea na motokari moja wa punda.
Baba na mtoto wake walijikumbatia na walilia juu ya furaha. Mfalme Faraoni aliwapokelea na sifa mingi na aliwapatia fasi moja juu ya kubakia kutumika.

Yakobo wakati alikuwa na miaka 147, alisikia ya kama anafika ku mwisho ya uzima wake, aliita watoto wake, aliwashauria kuchunga Imani ya Mungu wa kweli na aliwabarikia. Wakati alibarikia mtoto wake Yuda alimwambia sauti moja ya kama atazaliwa Mwokozi wa dunia toka watu wa kabila lake. Wakati Yakobo alikufa walimzika Kanaani.

Kiisha lufu yake, watoto wa Yakobo walibakia Misri pamoja na Yosefu. Watu wa kizazi chao waliogezeka na walifanya taifa moja jina lake Izraeli. Hii wakati walibakia Misri walikuwa wakiabudu Mungu wa kweli. Walikuwa wakikumbuka kula mara ile malako Mungu Aliwapatia wakubwa wao na kabisa kabisa ya kama siku moja watarudia mu inchi ya Kanaani.

**MAULIZO**

1. - Juu ya nini Mungu alichunga Yosefu fasi zote na wakati wote?
2. - Namna gani Yakobo alisikia tangazo ya kama anaishi Yosefu mtoto yake ?
3. - Namna gani waliishi Misri Yakobo na watoto wake ?

# KIPINDI CHA TATU

## Hadisi ya Musa ma Yesu wa Navihi

## 1. - Matangulizi

Kisha lufu yake Yosefu, watu wa Izraeli waliishi miaka mingi vizuri sana kule Misri. Hii taifa ilikuwa na makabila kumi na mbili iliyojenga miji yao.

Watu wa Misri waliwachukia kwa sababu walifuata Dini ingine. Kisha waliwaogopa kwa sababu waliwaza ya kama kuko namna ya hii taifa kubeba uwezo wa inchi yao. Juu ya hii mambo, mtumishi moja wa Faraoni aliwaza namna ya kuweza kusimamisha uzao wa watu wa Izraeli. Basi aliwapatia amri wale wanawake Wa ebrania waliokuwa wanasaidia wamama Waebrania wakati wa kuzaa, kuua watoto wote watakaozaliwa wanaume.

Mwanzo wakubwa wa Misri walikaza watu wa Izraeli kutumika nguvu sana. Kwa mfano kujenga vilalo, kuta na kufanya kila kazi ya nguvu. Ni hii wakati walijenga minara (pyramides) ya Misri iliyo makaburi ya Wafaraoni. Lakini watu wa Izraeli walizidi kuongezeka. Kisha Faraoni aliwaza namna ingine ya kuweza kuwaua. Alirubusu maaskari wake juu ya kubamba kila mtoto mwanaume na kumtupa mu mtoni Nili.

Hii mateso ilileta kitubio (repentence) kwa watu wa Izraeli kwa sababu walisahau Mungu wao wa kweli. Mungu alisikia kutubu kwao na alikamata mipango ingine juu ya kuwachunga na kuwaokoa mu hii uzima wao wa utumwa wa Misri.

## 2. - Wito wa Musa juu ya kuokoa taifa lake

Ile wakati alizaliwa mtoto moja aliyejaliwa neema, mama yake aliwaza namna gani atamuokoa. Alifichika ndani ya nyumba yake muda wa miezi tatu. Lakini kisha ilikuwa kweli hatari ya kumchunga juu ya mambo ya kulia.

Aliweza kufanye nini? Basi akabeba kitunga kimoja akakipakaa kabulimbo ndani, akamuweka mtoto wake ndani na akaacha kitunga juu ya mtoni Nili, pa fasi mtoto mwanmuke wa Faraoni alizoea kunawa maji. Kule karibu alijongea, kulifichama dada mkubwa wa Musa jina lake Mariamu juu ya kuangalia mambo gani itafanyika.

Kisha muda kidogo binti wa Faraoni alikuja pamoja na wasaidizi wake kunawa maji. Wakati alisikia mtoto eko analia ndani ya kitunga, alionyesha wabinti wengine kubamba kile kitunga na kukifungua. Pale aliona mtoto, alimpenda sana na alikamata mipango ya kumpeleka kwake na kule atamsaidia namna ya kumukomeshe.

Hii saa Mariamu alifika mbio sawa vile mama yake alivyomushauria. Alifika mbele ya ule mtoto wa Faraoni na alimuuliza kama iko lazima mwanamke moja aje kusaidia mtoto kwa sababu yeye alijua moja. Mtoto wa Faraoni aliitika na mara moja mama wa mtoto Musa alifika. Akamunyonyesha na kumbembelesha na kisha alienda naye kwake. Wakati mtoto wake alikomea, alimpeleka ku nyumba ya mfalme Faraoni, pale alijifunza na kupata akili mingi. Mtoto wa Faraoni alimpenda sana huyu mtoto na alimpatia jina la Musa, maana yake aliyeokolewa mu maji.

Musa alikomea nyumbani ya mfalme Faraoni, lakini hakusahau ndugu zake wa Izraeli. Wakati aliona mateso ndugu zake walianza kupata, alisikia mapendo mingi kwao na huruma mingi.

Aliwasaidia na kuwachunga daima. Siku moja mukutembea aliona mtu moja wa Misri kupiga mmoja wa kabila la Izraeli. Alisimama na kuuliza juu ya kusikia namna gani hii mambo inawafikia. Ule mtu wa Misri katika kasirani yake alitaka kupiga Musa. Basi, Musa akampiga huyu mu Misri.

Hii mambo haikubakie siri : Ni hivi Musa aliogopa ya kama mara ingine watu wa Misri watampiga. Alitoka mu hii mgini na kwenda mu inchi moja ingine jina lake Madiami. Kule alioa binti moja wa padri Lothori. Japo hiyo Musa hakusahau ndugu zake waliokuwa wanateswa na watu wa Misri. Hasikuache kuabudu Mungu wa kweli na kumuomba juu ya kumtosha Misri.

Siku moja, wakati alikuwa akichuga mashamba na kondoo ya muko (baba wa bibi) wake, aliona mti na majani kuwaka moto bila kuungua. Wakati alikaribia alisikia sauti moja kumuambia.

- Ee Musa, Musa ! Simama. Hii fasi iko takatifu. Mimi niko Mungu wa wababu wako.
  Mara moja Musa alipiga magoti yake chini na alisikia sauti ya Mungu iliyoendelesha kusema hivi:
  -Mimi ninaona mateso gani inavumilia taifa langu kule Misri na ninakamata mipango ya kuitosha katika utumwa. Weye utakuwa mkubwa wake. Ujitayarishe basi na wende Misri kuikomboa. Kwenda mbele ya Faraoni umwambie apatie ruhusa taifa la Izraeli kurudia ku inchi yao. Kama anakataa umuambie ya kama atapata mateso mingi.
- Ee Bwana, Musa alimuambia na unyenyekevu, mimi sistahili hii kazi Unanituma. Mimi sijui kusema vizuri.
- Mimi nitakuwa saa yote karibu yako na nitakupatia nguvu yangu, (hii sauti Ilianza kutoka ndani ya mti). Beba msaidizi wako ndugu yako Aaroni kwa sababu yeye anajua kuhubiri na kusumbulia vizuri. Yeye atakuwa na nguvu na ulinzi wangu.

**MAULIZO**

1. - Namna gani Faraoni alitaka kutesa na kuua watu wa Izraeili?
2. - Namna gani aliokoa Musa ?
3. - Muujiza gani aliona Musa wakati alikuwa anachunga kondoo za muko wake?

## 3. - Kutoka kwa Taifa la Izraeli Misri na kuvuka kwa Bahari Nyekundu

Musa pamoja na ndugu yake Aaroni walifanya sawa vile Mungu alivyowahamuru. Wakati walifika Misri, walienda mbele ya Faraoni aliyekataa kuwaacha waondoke na kuwaonyesha wakubwa wake wa kazi juu ya kutumikisha zaidi kupita watu wa Izraeli.

Halafu Mungu alikasirika na aliapiza nguvu Faraoni na watu wa Misri kwa malipizi kumi.

Moja yao, ilikuwa lufu ya kila mtoto wa kwanza mwanaume wa kila jamaa. Lakini watoto wote wanaume wa kwanza wa Izraeli waliokolewa, kwa sababu, Malaika wa Mungu aliwashauria watu wa Izraeli kupakaa damu ku milango ya nyumba zao sawa alama ya msalaba. Ni hivi wakati huyu Malaika alipita kuua watoto wanaume wa kwanza wa wa Misri, alikuwa anatambuka hii nyumba iliyokuwa na alama ya msalaba.

Juu ya hii mateso iliyokuwa ya mwisho, watu wa Misri waliogopa na waliomba kwa Faraoni aache watu wa Izraeli waende kwao. Sawa vile naye Faraoni alipata sikitiko sana juu ya hii mateso kumi aliyopata, alikamata mipango ya kuacha hii Taifa kuondoka.

Wakati hii Taifa ilipata ruhusa ya kutoka Misri na kwenda Kanaani, iliongozwa na wakubwa wake: Musa na Aaroni. Mungu aliwaonyesha Waizraeli mu namna ya ajabu hii njia walipashwa kufuata.

Hii Taifa tangu kutoka Misri ilifanya jangwani miaka makumi inne. Na sasa Waizraeli wapo wanashangilia kutoka kwao Misri. Na hii mashangilio iko Paska yao maana yake: Kutoka mu mateso na kunigia mu furaha.

Hii Paska yao inaachana na Paska ya Kanisa yetu ya Orthodoksia kwa maana sisi tunakumbuka Ufufuo wa Bwana wetu Yetu Kristu aliyetukomboa mu utumwa wa zambi ya Shetani.

Pale Waizraeli walitoka Misri, Faraoni aliona ya kama inchi yake haikuwa tena na watu wakufanya kazi. Juu ya hii, mfalme huyu aliwaza kutubu. Mara moja alituma maaskari wengi juu ya kurudisha watu wa Izraeli ku mkongo. Wakati maaskari walikaribia, Waizraeli nao walikuwa karibu ya Bahari Nyekundu. Walikuwa kweli katika hatari kubwa. Lakini Mungu naye hakuwaachilia. Alifanya muujiza wake. Alimpa Musa amri ya kupiga bakora yake juu ya maji ya

hii Bahari. Mara moja maji ilijigawanya na njia ilifunguka katikati. Ni hivi watu wa Izraeli waliweza kuvuka pasipo kuzama.

Maaskari nao waliingia mu hii njia lakini Musa, wakati aliona ya kama Waizraeli wote walivuka, alipiga mara ingine bakora yake na maaskari wote wa Faraoni waliteketezwa Baharini kwani maji ilirudia pa fasi yake na kuwafunika.

Mwisho wake Taifa la Izraeli ilimtukuza Mungu kwa sababu aliwaokoa katika hii hatari kubwa. Ni hivi waliweza kuendelesha safari yao.

**MAULIZO**

1. - Mateso gani makubwa kupita ingine yote Faraoni aliwapatia Waizraeli?
2. - Fundisho gani tunaweza kukamata ku hii muujiza ilifanyika ku Bakhari Nyekundu?
3. - Maachanisho gani iko kati ya Paska ya Wakristiani na Paska ya Waizraeli?

## 4. - Maisha ya Taifa la Izraeli ndani ya jangwa

Kisha Bakhari Nyekundu, Taifa la Izraeli iliingia katika jangwa moja mnene. Vyakula vyao vilianza kumalizika. Ndani ya hii jaigwa hamukuwa kitu. Walipata mateso mingi juu ya njaa. Juu ya hii mambo walianza kusikitika na kufanya makelele mbele ya Mkubwa wao Musa. Walitamani kurudia Misri mara ingine.

Musa aliwaomba kubakia na kuchunga Imani yao. Na kweli Mungu aliwatumia ndege mingi na waliwabamba na waliwakula. Kisha Mungu aliangusha pia mane tamu iliyokuwe inawapatia nguvu. Watu wa Izraeli walikuwa wakiulizana kati yao: “Mana ni kusema: Ni nini? Kila asubui walikuwa waliokota hii mana na kuikula muda wa wakati walifanya jangwani.

Kisha wakati kidogo hawakuweza tena kupata maji. Walianza kuteswa na kiu na walianza kuuzi Musa. Kwa hii mambo Musa aliomba saidio kwa Mungu. Naye Mungu alimwambia Musa apige bakora yake mu jiwe moja iliyokuwa mu mlima moja jina lake Horivi na mara moja maji ilitoka. Taifa la Izraeli ilimshukuru Mungu. Wakanywa na wakaendelesha mwendo wao.

Vile vile na saidio la Mungu mpendwa , Waizraeli waligombana sana na kiu cha maji, njaa na mambo ingine ya nguvu.

Hii miujiza yote intuonyesha ya kama Mungu eko daima karibu yetu. Haipaswi sisi kupoteza kitumaini chetu mbele yake.

Kisha miezi tatu Taifa hii ilifika mu mlima moja jina lake Sinahi. Kule walijenga mahema yao juu ya kupumzika. Basi Musa akapanda juu yake. Na kule alisikia sauti ya Mungu Ikimwambia hivi:

-Sema kwa watu Izraeli wakumbuke mara ngapi niliwalinda mpaka sasa. Kama wanasikia na kutimiza Mapenzi yangu nitawafanye kuwa Taifa langu pendelevu kupita mataifa mengine. Katika mateso na hatari yao watapata ulinzi wangu. Kama wanataka daima ulinzi wangu, inafaa kutimiza amri zangu ile miye nitawapatie.

Wakati Musa alishuka ku Mlima Sinahi aliwaambia watu kunawa, kufunga chakula siku tatu na kuepuka kila zambi na vile watakuwa tayari juu ya kukamata Amri za Mungu.

Siku ya tatu aliwaambia wafike chini karibu ya Mlima.

**MAULIZO**

1. - Namna gani Mungu alilinda watu wa Izraeli ?
2. - Tunafundiswa nini juu ya aapendo ya Mungu mbele ya watu ?

## 5. - Amri ya Mungu

Kisha wakati kidogo ilianza, juu ya Mlima, kuonekana mwangaza na makelele ya radi. Mlima huu ulianza kutosha shimoko. Sauti ya trompeti ilisililika na mwangaza wa radi ulionekana. Hii saa Taifa la Mungu iliona na ilisikia hile mambo ya ajabu ya Mungu na mara moja watu wa Izraeli walisikia Sauti ya Mungu mwenyewe aliyeanza kuwapatia Amri zake Kumi.

1. - Mimi niko Mungu wako na hakuna Mungu mwengine mpaka Mimi.
2. - Usisujudu sanamu na usiabudu viumbe vya Mungu.
3. - Usifanye malako bila neno na usitaje bure Jina la Mungu.
4. - Utatumika siku sita, hii siku ya saba utatukuza Mungu na utapumzika.
5. - Utasifu na utaheshimu wazazi wako juu uishi miaka mingi na ukuwe na furaha.
6. - Usiuwe ndugu yako hata moja.
7. - Utasifu na utaheshimu ndugu yako.
8. - Usiibe vitu vya ndugu yako.
9. - Usiseme sauti ya uongo wakati upo unasimulia na ndugu yako mwengine.
10. - Usitamani vitu vya ndugu yako.

Hii amri zote iko yenyi kufahamiwa na jina lao ni Dekalogos, nikusema Amri wa kumi.

Wakati watu wa Izraeli walisikia hii amri za Mungu walimlaka Mungu ya kama watatimiza hii amri katika uzima wao. Hivi ilifanyika masikilizano kati ya Mungu na Taifa lake na jina lake ni Agano la Kale.

Mungu alionekana na Amri zake ni mapenzi yake.

Kisha Musa alipanda mara ya pili ku Mlima Sinahi. Kule alibakia kwa kusikiliza Sauti ya Mungu.

Hii wakati Mungu alikuwa juu ya Mlima, Taifa la Izraeli ilisahau malako yake yale alilaka mbele ya Mungu. Basi, waliomba Aaroni afanye sanamu moja sawa vile ilikuwa kule Misri juu ya kuiabudu. Aaroni juu ya makankamisho yao, aliwafanyizia ngombe moja wa chuma. Aliiweka pa fasi moja ya juu na watu wa Izraeli walianza kuja kutoa mbele ya hii ngombe sadaka na nyama na walianza kuisujudu sawa Mungu wao.

Kiisha siku kumi na inne alishuka ku Mlima na alikamata mikononi mwake majiwe mawili juu ya ile Mungu aliandika Amri zake.

Wakati Musa aliona ndugu zake kusujudu huyu ngombe, alisikitika mingi ya ile kibengo yao walifanya na alitupa chini ile majiwe ya Amri juu ya kasirani yake. Ni hivi ilipasuka. Kisha Mungu alipoona hii ngombe aliapiza Taifa lake. Kwa sababu hii watu wengi walikufa kwani waliacha Imani yao mbele ya Mungu. Kisha hii mambo Taifa ilitubu na ilianza kuabudu Mungu wa kweli.

Musa alipanda mara ya tatu ku Mlima. Aliomba huruma kwa Mungu na alibeba majiwe ingine ya pili iliyokuwa na maandiko ya Amri juu yao.

Hii Amri aliiweka ndani ya sanduku moja ya mbao na hii iliitwa: “Sanduku ya Masikilizano”. Waliita hivi kwani ndani yake ilikuwa hii masilililizano ilitofanyika kati ya Mungu na taifa lake.

Katika safari yao, Wapadri wa Taifa walibeba hii Sanduku Takatifu juu ya mabega yao. Wakati walikuwa wanasimama kwa kupumzika kidogo walianza kuiweka ndani ya nyumba moja ya hema ilioitwa: “Hema ya Ushuhuda”, kwani ilichunga Sanduku ya Masikilizano yenye ilionyesha Mapenzi ya Mungu.

Taifa la Izraeli ilibakia ku Mlima Sinahi karibu mwaka moja. Kiisha walitembea mu fasi ya Kanaani. Kwa safari yao ndani ya jangwa Mungu aliwalinda. Lakini wao mara mingi walipoteza imani yao mbele ya Mungu na walifanya fujo mbele ya Musa.

Kama walipoteza kitumaini chao ni juu walisahau Mungu na ile miujiza alifanya kwa ajili ya mapendo aliyokuwa nayo kwao. Kila wakati walianguka na kusahau Mungu, mara moja, Mungu aliwaapiza na malipizi hiyo ilikuwa mingi na ya kuachana.

Wakati mija, nyoka mingi yenyi sumu ilifika kuumiza watu wa Izraeli na wengi walikufa. Musa aliwambia wasimamishe katikati ya fasi ya maaskari wao nyoka moja ya shaba. Na

aliomba wale wote walioumizwa na nyoka kuangalia ku ule nyoka ya chuma juu wapone. Hii nyoka ya shaba ilikuwa sawa mfano wa Bwana wetu Yesu Kristu aliyepanda pa Msalaba. Na sawa vile wa Izraeli waliponyeshwa wakati waliangalia ule nyoka wa chuma vile vile Yesu Kristu Anaokoa kila mtu anamuamini na anamufuata.

Wakati Musa alisikia mwisho wake, aliita wakubwa wa Izraeli juu ya kuwapatia mashauri yake ya mwisho. Aliwafafanusha mara ya mwisho Sheria ya Mungu, aliwaambia walichunge na wabakie katika aapenzi ya Mungu. Aliwahakikisha ya kama Mungu na ulinzi wake utawastahilisha kufika ku inchi yao Kanaani.

Musa kwa kuwa alikuwa Nabii, kwa njia ya Nuru Takatifu aliwaambia kufika kwa Mwokozi wa dunia. Ni kusema aliwaelezea tangu ile wakati ya kawa Yesu Kristu Atazaliwa toka Taifa lao na atatosha dunia mu uzima wa zambi.

Kisha, na Amri za Mungu, aliweka sawa mfuasi wake na mkubwa wa Taifa la Izraeli mtu moja jina lake Yesu  wa Navii aliyekuwa mtu wa akili na fazila. Kisha alipanda ku hii mlima iliyokuwa karibu. Aliangalia hii inchi Kanaanui, ikuwa mbali. Aliangalia pia ile fasi Taifa la Izraeli takaa siku zote katika malako ya Mungu. Alitukuza Mungu mara ingine na alikufa na miaka yake 120. Watu wa Izraeli walisikitika sana ya hii lufu ya Mkubwa wao. Walimzika na heshima mingi na walimlia muda wa siku 30 sawa vile ilikuwa desturi kwa mkubwa moja mpendwa na mbebaji wa Mwangaza.

**MAULIZO**

1. - Munakumbuka amri Kumi ya Mungu ?
2. - Nini ilikuwa Masikilizano ya zamani kati ya Mungu na Taifa lake?
3. - Nini ilikuwa Hema ya Ushuhuda.
4. - Ile nyoka ya chuma ni mfano wa kitu gani?

## 6. - Yesua wa Navii

Yesua wa Navii alizaliwa Misri mu ile miaka Taifa la Izraeli ilikuwa mu utumwa wa mfalme wa Misri. Alijua vizuri ile mateso ya Taifa na alitaka kuisaidia.

Ya hii mambo alikuwa msaidizi wa Musa. Alipenda inchi yake sana. Alikuwa mwenyi haki na nguvu na alikuwa na imani kwa Mungu. Kisha lufu yake Musa, Mungu Alifika kwa Yesu wa Navii na alimuambia:

- Sawa vile Musa alikufa, weye beba Taifa langu, vuka mtoni Yordani na kwenda ile fasi niliomiaga. Hakuna hata mtu moja atakaye mifungia njia. mpaka vile nilisaidia na nililinda Musa mpaka vile nitalinda weye.
  Mimi ninataka kusoma Amri zangu, kufanya mapenzi yangu na yote mambo ile itakuwa mazuri.
  
  Taifa la Izraeli pamoja na Mkubwa wao Yesua Navii walianza kwenda Kanaani. Mapadri walikuwa mbele, kiisha mkubwa wao na mwisho taifa mzima. Vile walitambuka mtoni Yordani mu namna ya ajabu sawa vile zamani walitambuka bakhari Nyekundu bila kulowana.
  
  Ile wakati walikaribia fasi ya Kanaani, juu ya kuikamata, walifanya vita kubwa kabisa. Mji wa kwanza kukutanisha ulikuwa Yeriko, uliozungukwa na ukuta mrefu pembeni yake. Yesua wa Navii aliukamata mu namna ya astajabu.
  
  Kiisha walifika mu mji wa Gavaoni na walianza vita na maskari wake. Karibu ya usiku vita ilikuwa bado kuisha. Ni vile Yesua wa Navii alimuomba Mungu kusimamisha jua juu ya kuisha hii vita. Na hivi ilifanyika mpaka vile. Jua ilisimama na Yesu wa navii alishinda maskari wa hii mji wa Gavaoni.
  
  Mwisho ilifika ile siku mbarikiwa ya watu wa Izraeli, waliingia mu hii fasi yao pendelevu. Ilikuwa kupitisha kwa miaka makumi inne tangu ile siku walitike Misri.

Wakati walikaa ku fasi ya wababu wao walimshukuru Mungu ya hii ulinzi wake. Kisha waligawanya hii fasi mu vipande kumi na viwili kufuatana na makabila yao kumi na mbili ya Izraeli.

Wakati Yesua wa Navii alisikia mwisho yake inakaribia aliita Taifa lake na aliishauria kubakia bila mitego siku zote katika Imani ya Mungu wa kweli na kutimiza amri zake. Mwisho alikufa na kipimo jia miaka 110. Alichunga imani yake na shukrani yake mbele ya Mungu na mapendo yake mbele ya Taifa la Izraeli.



# KIPINDI CHA INNE

## Hadisi ya Waamuzi

### 1. - Kuingia

Kiisha lufu ya Yesu wa Navii, watu wa Izraeli walianza kutembea pamoja na wale wenye sanamu. Walisahau Mungu wao wa kweli. Waliabudu nao sanamu sawa wale wenye sanamu. Kwa hii mambo Mungu aliwaapiza Akiacha waadui wao wale walikaa kule pembeni yao kuja kuwaua na kuwaletea mateso. Wakati waadui wao walikuwa wanawatesa, wao walianza kutubu na kugeuza mifano yao mibaya na waliomba ulinzi wa Mungu wa kweli. Mungu mpenda wanadamu aliwasamehe na aliwatuma wanaume wa heshima ya Mungu na nguvu ya vita juu ya kuwaokoa. Wao wanaume walikuwa kwa miaka ya vita yao sawa wakubwa wao na kwa wakati wa amani yao, walikuwa wachungaji wao. Wao walihukumu watu wao na ya hii mambo waliitwa Waamuzi.

### 2. - GEDEONI

Gedeoni alikuwa mtu moja wa mgini uliokuwa na heshima mingi mbele ya Mungu na nguvu ya vita. Siku moja yeye alibeba Amri ya Mungu juu ya kukomboa Taifa la Izraeli ku adui moja jina lake Madianiteni. Wale waadui walitesa na waligombanisha kwa vita kali ile Taifa la Izraeli. Hii wakati Gedeoni alibeba waaskari makumi tatu elfu (30. 000) na alienda kupiga waadui wake wa Madianiteni. Na Amri za Mungu, alichagua mpaka watu mia tatu (300) kati ya maaskari makumi tatu elfu wale walikuwa nguvu mingi. Na ni hawa waliopigamaadui wao. Aliwaambia kubeba ya udongo na tanumbela moja? Ndani ya birika waliweka mushumaa (bougie) moja ya moto. Kiisha aliwaachanisha mu vipande tatu na wote walikuwa tayari kwa kupiga waadui.

- Aliwaambia hivi: hii kazi tutafanya mweye na miye, na saidio la Mungu tutamshinda adui wetu.

Wakati walikaribia ile fasi walikuwa maadui wao ilikuwa katikati ya usiku na watu wa Madiniteni walilala sana.

Gedeoni, bila kupoteza wakati, aliingia ndani ya hii fasi na maaskari wa adui wao na ile tarumbeta ililia nguvu. Alipasua birika yake, aliinua juu ile mshumaa na alipatia maaskari wake alama ya kuanza vita. Maaskari wake wote walimfuata. Walipasua mabirika yao, walikamata mishumaa yao ku mukono moja na ku mkono ingine walikamata tarumbeta yao na waliangukia maadui.

Taifa la Madianiteni, wakati ilisikia malalamiko yao na kuona moto ya mikono yao, iliogopa na ilikimbia juu iokolewe. Gedeoni aliifukuza pamoja na maaskari wake na aliharibu kundi la maaskari wake.

Ushindi wa Gedeoni ulikuwa munene sana. Taifa iliishi na furaha na ilitukuza Mungu juu ya hii wokovu wake.

**MAULIZO**:

1. Wanani waliitwa Waamuzi?
2. Namna gani Mungu alisaidia taifa la Israeli waakti ilikuwa inatubu?
3. Namna gani Gedeoni alishinda maadui wake?

# 3. SAMSONI

Kisha kifo cha Gedeoni Waisraeli walianza mara ingine kusahau Mungu wa kweli. Walianza kutembea pamoja na watu wa sanamu na walianza kuabudu sanamu zao. Mungu aliwaapiza mara ingine na aliwaacha maadui wengine kuwashinda na kuwavuka utumwa. JIna la maadui wao ilikuwa Filistini.

Taifa la Israeli ilibakia katika utumwa wa Filistini makumi inne. Juu ya ile mateso yao walitubu na waliomba saidio la Mungu. Mungu mwenye Mwema aliwasamahe mara ingine na alituma juu ya wokovu wao mkubwa Sapsoni.

Samsoni aliishi tangu udogo wake na heshima ya Mungu na alikuwa na nguvu mingi mwilini mwake.

Huyu alileta woga na matetemeko mbele ya Wafilistini nao walitafuta wakati gani juu ya kumuua. Siku moja walifichama inje ya nyumba moja ya pori pale alipanga usiku. Wambamba na walimfunga. Lakini Samsoni alikata mnyororo wake, aliwafukuza na aliwapatia mateso mengi.

Watu wa Filistini walisikitika kwani hawakuweza kumuua Samsoni. Ile wakati mwanamuke moja, jina lake Dalida alimtoa. Alisikia ya kama nguvu ya ajabu ya Samsoni inatoka ya nywele yake. Juu ya hii mambo wakati alilala huyu mwanamuke alimkata nywele yake na alimfunga. Kisha walimtosha macho yake na walimtupa ndani ya gereza.

Siku moja Wafilistini walikuwa na siku Kuu mkubwa ya huyu Mungu wa uwongo wa kabila lao. Kule ndani ya kanisa yao walikuwa wote pamoja karibu elfu tatu na walimleta Samsoni. Walimfunga katikati ya nguzo mbili na walimchokoza. Samsoni, sawa hakuweze kuvumilia tena, alifanya sala ndani ta roho yake na akili yake mbele ya Mungu. Kisha alimuomba kumsamehe zambi zake na kumsaidia juu ya kuapiza maadui wake. Kisha alikumbatia ile nguzo mbili iliyosimamisha nguvu ile nyumba na alisema na sauti ya nguvu: «Mimi ninakufa sasa pamoja na maadui wangu». Alipomoa kabisa nguzo yote mbili hata paa ya nyumba ilianguka na wafu wote waliokuwa ndani ya hii nyumba walikufa pamoja na Samsoni.

**MAULIZO**:
1. Namna gani Mungu alisaidia Samsoni mbele ya Wafilistini na juu ya nini?
2. Namna gani Wafilistini walimbamba na walimfunga Samsoni?

# 4. ELIA

Kisha Samsoni, Mwamuzi mkubwa wa taifa la Israeli alikuwa Elia, mwenye alikuwa askofu wao.

Elia alikuwa mtu wa heshima mbele ya Mungu, lakini alikuwa na watoto wake wawili wenye hawakuwe wazuri na hawakuwe na heshima mbele ya Mungu. Walizarau Amri za Mungu na mifano yao mbele ya wakubwa ilikuwa mibaya.

Mara mingi Elia alishauria juu ya kusaidia watoto wake kugeuza mifano yao. Lakini yeye, sawa vile alikuwa mtu mwema mno na alipenda watoto wake kuliko Mungu, alikataa kuwashauria na kuwaapiza ya kila kosa lao na vile walibakia bila kutubu na kugeuza mifano yao. Mungu alimwambia Elia ya kama watoto wake watamletea mambo mabaya ya uzima wake na hivi ilifanyika.

Kwa ile vita watu wa Israeli walifanya mbele ya Wafilistini walipata uharibifu mingi. Ku vita moja watu wengi walikufa na katikati yao walikufa watoto wa Elia. Tena Waisraeli walipoteza na Sandugu la Masikilizano, kwa sababu maadui wao waliibeba.

Elia, baba yao, wakati alisikia mateso ya taifa la Israeli, alishangaa, alitetemeka na alianguka chini sawa mfu.

## 5. Samueli

Kisha kifo cha Elia, Samueli aligeuka mkubwa wa Israeli. Yeye ni wa mwisho ku wakubwa wa Waebrania. Samueli alizaliwa kisha maombi mengi ya wazazi wake wenye hawakuweze kuzaa watoto tangu udogo wake alipenda kuingia mu Misa na kubakia karibu ya Elia, askofu wa hii Kanisa. Alikuwa mtu wa fazila na waheshima. Alimpenda na alimwabudu Mungu na roho yake nzima.

Na ya hii mambo alibeba kwa Mungu zawadi ya kuwa Nabii. Waebrania walisikia sauti yake na heshima mingi.

Samueli, waakti alifanyika Mkubwa wao alitaka kuleta uhuru kwa watu wa Israeli ya maadui wao Wafilistini, kwa hivi aliwaita na aliwaelezea hivi: «Mutubu! Mukumbuke mara ingine Mungu. Mutimize Amri Zake na Yeye atamipatia uhuru ya maadui wenu.

Watu wa Israeli walisikia Samueli. Walitubu kweli na waliomba saidio la Mungu. Na mkubwa wao Samueli, walipigana vita hata kushinda maaduni wao Wafilistini na mwisho walibeba mara ingine Sandugu ya Masikilizano. Tangu ile wakati Wafilistini hawakuuzi tena na waliishi na amani.

Samueli alikuwa mkubwa wao muda wa miaka makumi mbili na watu wa Israeli waliona siku za utukufu na za furaha.

Wakati, Samueli alizeeka alitumika mpaka kazi ya Kiaskofu kwao. Watoto wake wawili walifanyiwa kuwa waamuzi. Lakini sawa vile watoto wake hawakuwa wengi haki na imani, Waebrania walimuomba Samueli achague mfalme sawa vile mataifa ingine pempeni yao ilikuwa. Samueli basi, na baraka ya Mungu, aliweka Saulu sawa mfalme wao wa kwanza, mwenye alikuwa na fazila na nguvu ya mwili.

## 6. Ruta.

Ile wakati Waamzi walikuwa wakubwa wa taifa la Ebrania, mateso mingi ilifika ku fasi yao. Watu mingi walikimbia inchi yao. Walienda ku fasi ya kigeni juu ya kupata kazi na chakula hivi wapate kuishi. Moja kati yao alikuwa Elimeleki mwenye alizaliwa mu mgini Bethleemu wa Yudea.

Elimeleki alibeba bibi yake Noemi na watoto wake wawili na alienda kufasi ingine ya karibu, ile inaitwa Moabu. Elimeleki kisha miaka kidogo alikufa. Bibi yake Noemi aliwaoeya watoto wake wabibi wa fasi ya kigeni. Moja alioa Orpa na mwengine Ruta. lakini hawakupitisha wakati mingi na watoto wake Noemi walikufa. Basi mwisho, Noemi alikamata mpango wa kurudia kufasi yake, karibu ya majirani wake. Moja bibi wa mtoto wake Orpa alirudia kwa jerani na ndugu zake. Lakini ule mwengine Ruta, mwenye alikuwa mzuri sana na aliyependa muko wake, alikataa kumuacha hivi na kutoka. Alitaka kumsaidia na kutumika pamoja naye kwa sababu Noemi alikuwa mzee.

Alimwambia: Mama, usinishurutishe kukuacha na kurudia. Ile fasi wewe utaenda na miye nitakufata. Mungu wako atakuwa Mungu wangu na kabila lako itakuwa kabila langu. Mpaka lufu njo itatuachanisha.

Noemi, pakuona ile mapendo ya Ruta, alimbeba karibu yake. Pamoja naye walirudia ku mgini Bethleemu. Ile wakati ilikuwa waakti wa mavuno na chakula ilionekana ya mingi.


Ruta kila siku alienda mashambani ya mtajiri moja mlimaji mwenye aliitwa Boozi, jirani wa Noemi. Kule Ruta aliokota majani pamoja na mbegu ya ngano juu ya kula yeye na muko yake Noemi. Ile wakati kulikuwa zoezo moja nzuri juu watu maskini waliweza kutoka inje juu ya kwenda kuokota ndani ya mashamba ile ngano iko inabakia ku mwisho ya mavuno kufuatana na sheria ya Mungu.

Boozi aliyekuwa mtu mzuri na wa heshima, alitangaza hii mfano na uzima wa Ruta. Alimsifu juu ya mfano wake na alimuomba kumuoa. Na vile ilifanyika. Na ni ku hiki kizazi cha

Boozi na Ruta kulitoka Daudi, mwenye aliyefanya mfalme wa Waebrania na katika kabila lake alizaliwa Bwana Yesu Kristu. Vile Ruta mfazili alistahiliswa kuzaliwa mu kizazi chake, kisha miaka mingi, Yesu Kristu.

**MAULIZO**:

1. Juu ya nini Ruta hakutake kuacha muko wake?
2. Namna gani Ruta alibeba malipo ya roho juu ya ile mapendo na heshima yake?



# KIPINDI CHA TANO

## WAFALME.

### 1. Saulo

Saulo alikuwa mfalme wa kwanza Waebrania. MBele kidogo ya wakati, alifuata mashauri ya Samueli na alitumika vizuri. Alikuwa mfalme katika mapenzi ya Mungu na alitumika na haki na heshima. Ni hivi hata taifa lake aliichunga katika njia ya kweli na alichunga vizuri pia inchi yake ku maadui wake na alileta uhuru mu inchi yake.

Lakini hii kazi nzuri yake ilileta majivuno ku roho ya Saulo. Juu ya majivuno yake alifanya kazi ile alitaka na hakupende kutengeneza kila mambo yake na haki na ukweli. Tena alianza kukataa kuheshimu Mungu na alipenda kukanyanga Amri Zake.

Samueli alipata sikitiko rohoni mwake kwani Saulo hakuwa tena na heshima kwa Mungu na aligeuka mfalme asiyestahili. Mara mingi Samueli alimwambia ya kama mifano yake inaleta mateso ku taifa lake. Tena alimuonyesha ya kama Mungu atamuapiza juu ya hii majivuno na kiburi chake. Lakini aligombana ya bure juu ya kumsaidia ili apate kutengeneza mifano yake na kufuata njia ya Mungu. Saulo, wakati alisikia mashauri ya Samueli wakati kidogo, alitubu. Lakini alianguka mara ingine katika zambi. Vile siku kwa siku aligeuka mbaya kuliko mtu mwenye mbaya na aliishi na sikitiko mingi, kwa sababu hakuwe karibu yake Mungu. Tena wakati alisikia ya kama iko namna ya kupoteza kiti chake juu ya zambi zake, alipata sikitiko mingi na alikata kitumaini chake. Hii wakati waliwaza kuleta ku nyumba ya mfalme kijana moja mwengine sawa mfalme wao jina lake Daudi aliyekuwa mchungaji wa kondoo n alikuwa anajuwa kucheza vizuri sana kinubi kimoja na alileta furaha ku nyumba ya mfalme na hii nyimbo zake.

**MAULIZO**:

1. Mambo gani ilitoka juu ya majivuno ya Saulo?
2. Nani alisaidia Saulo mu waakti wake mbaya?

### 2. Daudi na Goliathi.

Daudi alikuwa kijana bila woga na alikuwa na roho ya nguvu kabisa. Ile nguvu yake tunaiona kabisa mu hii mambo inafuata.

Watu wa Israeli walikuwa vita na Wafilistini. Hii makundi wawili ilikuwa tayari ya vita hiyo. Mara moja mu kundi la maaskari wa Wafilistini mulitoka askari moja mnene na wa nguvu kabisa aliyeitwa Goliathi na aliita na majivuno na zarau ile kundi la maaskari wa Israeli hivi: «Kama katikati yenu moja anataka kufanya ugonvi na miye sasa anaweza kufika. Kama moja katikati ya sisi anapata ushindi, kundi la maaskari wake itapata hii ushindi.

Lakini hata askari moja wa kundi la Ebrania hakutake kufanya ugonvi na huyu Goliathi aliyeendelesha, muda wa siku makumi inne, kuita na kuchambula watu wa Ebrania na dini yao. Maaskari wote wa Ebrania walipata woga na matetemeko.

Asubui moja alifika ku kundi ya maaskari wa Ebrania kijana moja aliyekuwa mchungaji wa kondoo jina lake Daudi. Alifika kule juu ya kuangalia ndugu zake wenye walikuwa maaskari. Ile saa alisikia sauti ya Golioathi aliyeita maaskari wa Israeli kugombana nao.

Daudi, wakati alisikia hii sauti yake, alisikia haya mnene. Alifika mbele ya mfalme Saulo na imani ya Mungu na alimuomba ampatie ruhusa juu ya kugombana ugonvi yeye mwenyewe na ule adui Goliathi. Kisha sala aliyefanya mbele ya Mungu, alibeba mpila moja na majiwe kidogo na alifika mbele ya Goliathi.

Wakati Goliathi alimuona, alicheka na alimwambia na zarau mingi: «Unawaza ya kama miye niko imbwa pale unakuja na hii mpila na majiwe kunipiga?»

Na Daudi aliyekuwa na amani kwa Mungu alimjibu hivi: «Wewe unakuja mbele yangu na bunduki mingi, kisu na mkuki, lakini miye ninakuja na saidio la Mungu ule uliyemzarau wewe sana.

Alimkaribia Daudi na yeye aliweka jiwe moja mu mpila wake na alimpiga pa sura yake na alimlalisha chini, kisha alitosha kisu ya Goliathi na alikata kichwa chake. Maaskari wa Ebrania walikamata nguvu na waliwafukuza maadui wao mbali ya inchi yao. Hii tendo la kuwaaida ya Daudi ilimletea sifa ya ajabu kwa ndugu zake.

**MAULIZO**:
1. Namna gani Daudi alimuua Goliathi?
2. Fundisho gani tunabeba ku ile tendo la Daudi?

## 3. Roho kubwa ya Daudi

Kisha ule ushindi walifanya mbele ya maadui wao, ni kusema wa Filistini, watu wengi wa Israeli walitoka inje ya nyumba zao juu ya kupiga mikono na kupokelea maaskari wao na walisema hivi: «Saulo alishinda ma elfu ya maadui, lakini Daudi alishinda makumi elfu ya mingi».

Saulo wakati aliona ya kama ndugu za Israeli walimtukuza Daudi kuliko yeye, alipata sikitiko. Tamaa iliingia ndani ya roho yake na alianza kumchukia Daudi. Aliogopa ya kama atapoteza kiti chake na cheo chake. Juu ya hii tamaa yake na chuki mbele yake alikamata mpango juu ya kumuua Daudi.
Daudi ile wakati alisikia ya kama uzima wake uko katika hatari. Alitoka ku nyumba ya mfalme pamoja na ndugu zake na aliishi mu pori.

Lakini Saulo hakuweze kupata ukimya na kule alimuvijia kummbamba. Watu mabaya walimwambia ya kama Daudi alitaka kubeba kiti chake na ya hii mambo yeye aliogopa na alimuvijia juu ya kumuua.

Lakini Daudi alimheshimu na alimpenda Saulo na hata saa moja hakuwaza kubeba kiti cha mfalme Saulo. Mara mingi ilifika wakati wa kuweza kuua Saulo, kama alitaka, lakini hakufanye ile. Alikuwa heshima sana mbele ya uzima wa mfalme hakutake kufanya kazi moja mbaya.

Mara moja Saulo alichoka na kuvijia Daudi, akalala kwa kupumzika mu nyumba moja ya pori. lakini ndani ya hii nyumba Daudi na marafiki wake walikuwa wanapumzika ku fasi moja ingine kidogo ya ndani zaidi. Ile wakati rafiki moja wa Daudi alimshauria abebe kisu kimoja na amuue mfalme Saulo, lakini yeye alikataa, kwa sababu alisema ya kama Mungu alimpatia Saulo hii kiti ya kutumika sawa mfalme wa watu wa Ebrania. Alikata mpaka kipande kimoja cha nguo ya mfalme, mwenye aliyekuwa analala ile wakati. Mara moja Daudi alitoka.

Na wakati ingine Daudi alimpata Saulo ku fasi moja wa kulala, lakini hakumfanya ubaya. Alimbeba mpaka mkuki wake na hii kopo alikuwa anakunywa nayo maji pasipo kumpiga ao kumuuzi. Kisha ya hii roho kubwa ya mapendo ya Daudi alimustajabu Saulo, lakini hakuacha kumfukuza juu ya kumuua.
Hakufanye siku nyingi na Mungu alimwapiza Saulo juu ya hii mfano wake mbaya.
Wakati moja alikuwa vita na Wafilistini, lakini watu wa Ebrania walipoteza nguvu yao na Wafilistini walikamata ushindi walimpiga Saulo na alipata vidonda vya nguvu. Na kwa sababu hii, aliogopa ya kama maadui wake watambamba na waatamtesa, alikata na kisu yeye mwenywewe shingo yake na alikufa. Katika hii vita walikufa watoto wake watatu. Moja kati yao alikuwa Yonatani aliyekuwa rafiki wa Daudi. Daudi aliuzika mingi rohoni mwake juu ile lufu ya rafiki yake na mateso ingine ilifanyika.
**ULIZO**:

1. Fundisho gani tunabeba ya ile mfano wa Daudi mbele ya Saulo?

## 4. Daudi anafanyiwa mfalme.

Kisha lufu ya Saulo Daudi aligeuka mfalme wa taifa la Israeli na miaka 30. Alitumika sawa mfalme na akili mingi na imani mbele ya Mungu. Kwa ile wakati yeye alikuwa mfalme, inchi yake ilipata nguvu mingi, sifa na utukufu mbele ya mataifa mengine.

Ya kwanza Daudi alitengeneza kundi la maaskari wake, aligombana na aliepuka maadui wa Israeli na alifanya Yerusalema kuwa mgini mkubwa wa inchi yake.

Daudi alikuwa na heshima mingi mbele ya Mungu. Mu Yerusalema alijenga nyumba moja nzuri na ndani yake alipeleka na aliweka Sanduku ya Masikilizano (Agano), ile alikamata ya mikono ya maadui wake. Wakati walipeleka hii Sanduku yao Takatifu Daudi alitembea mbele na mavazi yake meupe, aliimba na alicheza kinubi kimoja. Watu wengi walimfuata nao waliimba nyimbo za furaha za Dini yao pamoja na tarumbeta na filimbi.

Daudi alikuwa mshairi mkubwa. Aliandika zaburi mingi na nzuri na alicheza na kinubi chake. Zaburi yake yote iko 150, tupotunaisoma ao tunaiimba mpaka sasa mu Kanisa yetu.

Daudi lakini, wakati moja, alifanya zambi moja mnene. Na Mungu lakini alituma Nabii Natani, mwenye alimushauria na alimwambia ya kama, kama anakataa kutubu, Mungu atamuapiza juu ya hii zambi yake. Mashauri ya Natani ilimsaidia yeye kusikia zambi yake na alitubu kweli. Alifanya mafungo ya chakula na aliomba Mungu amusamehe. Kisha aliandika zaburi moja, ile ndani yake aliandika toba yake. Hii zaburi tunaisikia kila wakati mu Kanisa yetu. Iko zaburi 50 (51).

Daudi alikufa na kipimo cha miaka 70 sawa mfalme miaka 40.

Tazama kidogo mistari ya hii zaburi yake namba 50 (51):

Unirehemu, ee Mungu, sawa sawa na wema wako; sawa sawa na wingi wa rehema zako uzime makosa yangu.. . . Maana ninajua makosa yangu, na zambi yangu ni mbele yangu daima.. . . Ufiche uso wako usitazame zambi zangu, ee Mungu, na uzima maovu yangu yote.. . . . Ee Bwana ufungue midomo yangu na kinywa changu kitaonyesha sifa zako.

**MAULIZO**:

1. Fasi gani Daudi alipeleka Sanduku la Masikilizano (Agano) na juu ya nini?
2. Unajua nini ya hii zaburi ya Daudi?

## 5. Solomoni.

Kisha lufu ya daudi, Salomoni alipanda pa kiti cha ufalme wa Israeli. ALikuwa mfazili, mtu wa akili na wa heshima mbele ya Mungu.

Kisha sandaka yake moja, Mungu alifika ku usingizi yake na alimwambia: «Uniombe kitu gani unapenda». «Ee Bwana, Salomoni, alimjibu, unifanye mfalme wa taifa moja mnene. Miye lakini ningali kijana. Unipe, basi, hekima juu ya kutumikia na mapendo mingi na nuru yako taifa langu.

Mungu alifurahi ya hii sauti yake na alimjibu: «Na mwangaza mingi kwa akili yako mimi nitakupatia na utukufu mingi na mali mingi na utaishi miaka mingi».

Kweli Salomoni aliishi miaka mingi na alifanya matendo ya kawaida na alipata mali mingi. Alitumika sawa mfalme na hekima na haki. Alama moja ya akili yake iko hii:

Siku moja wanawake wawili walifika mbele yake na walimuomba kuwa fungulia mambo yao moja. Hawa waliishi pamoja nyumbani moja na siku moja walizaa wote wawili moto moja moja. Usiku moja, moja mwanamuke kati yao wakati alilala, alimlalia mtoto wake na alimuua

bila kutaka kufanya vile. Wakati huyu mama alipoamka, aliona ya kama mtoto wake amekwisha kufa, mara moja alibeba na alimuweka karibu ya mwenye zake na alibeba mtoto wa huyu mwengine na alimuweka karibu yake.

Asubui, wakati wote wawili waliamka walianza kufanya makelele, kwa sababu kila moja alisema ya kama huyu mtoto mzima ni wake. sawa vile hawakusikilizana, walikamata mpango wa kwenda kwa mfalme juu ya kuwapatia jibu.

Salomoni wakati alisikia mambo yao, hakukawia kufungua mambo hiyo. Alisema kwa askari moja kubeba huyu mtoto na kisu chake na amkate katikati na kisha mama achukue kipande chake kimoja.

Wakati, huyu mama wake wa kweli alisikia hii jibu, alilamika na kulia machozi akimwambia vile, iko vizuri basi wamupatie ule mama mwengine mtoto wake.

Salomoni alitaka kusikia mpaka hii sauti. Mu hii sauti ya sikitiko ya huyu mama Salomoni alisikia ya kama huyu mama eko kweli mama wa mtoto huyu. Na hivi aliweza kumpatia mtoto wake na mambo yao ikaisha.

**MAULIZO**:

1. Juu ya nini Mungu alimpatia Salomoni hekima mingi?
2. Wakati gani hekima ya Salomoni ilionekana?

## 6. Matendo ya Salomoni.

Ile miaka Salomoni alikuwa mfalme hata adui moja hakuuzi ufalme wake. Kwa hii mambo alifanya matendo mingi juu ya kusaidia taifa lake. Kazi yake ya kwanza na mnene kabisa ilikuwa wa ile Kanisa alijenga mu Yerusalema. Hii Kanisa aliijenga karibu miaka 2000 mbele ya kufika Bwana Yesu Kristu duniani. Juu ya hii Kanisa walitumia watumishi wajengaji wengi muda wa miaka saba. KUta za hii Kanisa zilikuwa za zahabu. katikati ya hii Kanisa kulikuwa nguo moja iliogawanya Kanisa mu vipande viwili: Vitu Vitakatifu na fasi ingine ya kanisa.

Wakati aliisha kazi ya hii Kanisa Salomoni alienda kuchukua Sanduku la Agano ku ile fasi yake aliiweka zamani na akatoa sadaka ya mingi. Wakati ile yote mapadri na taifa nzima walimtukuza Mungu na waliimba nyimbo za kuachana.

Ku mwisho Salomoni aliomba kwa Mungu unyenyekevu juu ya kulinda taifa lake vizuri. Kisha alibarikia taifa lake na aliishauria kuchunga imani mbele ya Mungu. Tangu ile wakati watu wa Ebrania walisadiki ya kama Mungu anakaa ndani ya hii Kanisa na ilipaswa kumuabudu mpaka ndani ya hii fasi.

Salomoni alifanya tena na matendo mengine. Alijenga na migini ingine na pempeni yao alijenga kuta. Hekima na utukufu yake ilitawanyika fasi zote za dunia na watu walifika kumuona na kumfahamia.

Salomoni aliandika vitabu vingi vyenye viko ndani ya Agano la kale. Sasa tutaleta hapa mpaka mafundisho kidogo ya hii Kitabu chake, Hekima ya Salomoni:

«Mwenye, wenye munatumika mu inchi yenu sawa wafalme inafaa kupenda haki. haki iko chemchem ya uzima wa milele».

«Nafsi ya watu wa heshima, Mungu anawalinzi na mtu hata moja hawezi kuwaharibisha».

«Ule mtu anayezarau shauri na mapendo ya ndugu yake eko mtu wa maombolezo na Mungu atamuapiza».

«Hekima iko sawa muwa ile haikauki. Nyingi munaipenda inafaa kuitafuta».

«Kila mtu anayetaka furaha kweli inafaa kupata hekima na hii itamletea mambo yote ya furaha».

**MAULIZO**:

1. Ni tendo gani nene la Salomoni inapita matendo yake mengine?
2. Juu ya nini Salomoni alikuwa mfalme mtukufu wa Ebrania?
3. Fundisho gani ya Kitabu kile cha Hekima inafurahisha kabisa?

## 7. Uharibisho wa ufalme wa Yudea na utumwa wao mu mgini Babilona.

Kisha lufu ya Salomoni, mfalme alikuwa mtoto wake Roboamu. Lakini yeye alizarau taifa na mifano yake mbele ya taifa ilikuwa mibaya. taifa la Ebrania basi ilifanya fujo na ilimtosha mpaka makabila mawili ya Yuda na ya Benzamini njoo walimfuata. Makabila mengine kumi ilichagua mfalme mwengine jina lake Yeroboamu.

Hivi ufalme wa Waebrania ilikatika mu vipande viwili. Kipande kimoja cha mfalme Roboamu kiliitwa ufalme wa Yuda na mgini wake mkubwa ulikuwa Yerusalema na kipande kingine kiliitwa ufalme wa Israeli na mgini wake mkubwa uliitwa Samaria.

Ile maachanisho ilileta uharibisho kwa ule ufalme moja wa zamani kwa sababu ilileta chuki katikati yao na mara mingi ufalme moja uligombanisha ufalme ingine na vile nguvu yao ilishuka sana. Na mambo ingine ya mbaya kabisa iko ya vile walisahau pole-pole Amri ya Mungu. Walifanya matendo mabaya na waliabudu sanamu. Ile wakati walionekana wale watu walioheshimia Mungu na walikuwa watumishi wa Mungu nao hawa waligombana na mashauri yao juu ya kurudisha jii taifa mu njia ya kweli. Lakini hakuna namna. Wao walikataa kutubu na walifanya mabaya kupita. Kisha wakati ingine walipoteza uhuru yao na waliishi watumwa wa mataifa ya kigeni. Ufalme wa Israeli na mfalme wake wa bila imani ulianguka mbio-mbuio katika imani ya sanamu na mara moja maaskari wake walikufa ku maadui wake.

Ufalme wa Yuda uliishi miaka mingi kupita, kwa sababu ilichunga Sheria ya Musa. Ilibakia ndani ya hii ufalme na kizazi ya Daudi, toka yake alikuja Kriatu duniani. Lakini na hii Ufalme ulianguka. Mfalme Roboamu alisahabu na yeye Mungu wa kweli na aliabudu ma sanamu na pamoja naye alikokota na taifa yake. Huyu walimufuata na wafwasi wake. Wakati kupita kibaya ulikuwa kile alitawala mfalme mwanamuke Gotholia na kisha mufalme mwanaume Manasis. Hawa wa wili waliuwa ma Nabii wingi, wenye walihubiri toba mu Taifa na warudie kwa Mungu. Lakini walikuwa na wafalme weshimiwa, sawa Yosafati, Yoathami, Ezekias na Yosias, lakini walishindwa kuokoa taifa toka uharibifu iliyokuja. Apizo ulikuja mnene mu ufalme ya Yuda. Ku mwaka 586 mbele ya kuzaliwa Kristu mufalme wa muji Babilona ya Pesria, aliyeitwa Nebukadneza wa pili alikamata muji Yerusalema na aliharabisha ufalme wa Yuda. Aliiba vitu ya Hekalu yao na aliuwa watu waIzraeli. Walimubamba mufalme Sedekias, walimutosha ma macho yako na walimupeleka mutumwa pamoja na watu wengine mujini Babilona.

**ULIZO**:

1. Hii uharibisho wa Wafalme wawili unafundisha nini?

## 8. Utumwa mu mji Babilona

Wale watu wa Yuda, wenye walipelekwa mu fasi ya utumwa mu inchi Persia, waliteswa na namna mbali mbali, wakati walitembea ku muji Babilona. Zaburi 136 (137) inatuonyesha hile mateso yao:

Zaburi 137:

Kandi ya mito ya Babeli, pale tuliketi, ndiyo, tukalia, wakati tulipokumbuka Sayuni. Katika miti iliyo katikati yake tukatundika vinubi vyetu. Maana kule waliotupeleka wafuingwa walitaka nyimbo kwetu, nao waliotuharibu walitaka furaha wakisema: Mutuimbie mumoja wa nyimbo za Sayuni. Tutaimba wimbo wa Bwana namna gani katika inchi ya ugeni? Kama nikikusahau, ee Yerusalema, mukona wangu wa kuume usahau akili zake. Ulimi wangu ufungane na upande wa juu wa kinywa changu, kama nisipokukumbuka; kama nisipotaka Yerusalema zaidi ya furaha yangu iliyo kubwa. Kumbuka, ee Bwana, juu ya wana wa Edomu, siku ya Yerusalema; waliosema: Mwobomoe, mwobomoe, hata kufika musingi wake. Ee binti ya Babeli, uliyeharibiwa; Heri atakayekulipisha kama wewe ulivyotutendea sisi. Heri yeye anayekamata wadogo wako na kuwatupa kwa nguvu juu ya mwamba.

Miaka wa wili wa kwanza waliteswa mingi. Waliisha kuzambalala ma fasi ya kuachana na waliisha katikati ya wageni, wenye walikuwa dini ingine na kutim ingine. Kisha miaka wa

wili uzima yao ilikuwa nzuri kupita. Mfalme Nebukadneza aliwapatia cheo ya kuwa watu ya inchi yake. Hawa walitumika sasa na uhuru na wengine walipanda ma cheo kabisa wa juu. Tena walianza kusaidia na wa ndugu wao, waliwaacha mu Yerusalema.

Wale watoto wao, wenye walizaliwa mu Babilona, hawakujua lugha yao wa ebrania, kwani walijua lugha ya taifa ya Babilona, iliyoitwa Aramea. Kwa hivi, hile lugha walisuburia wale watu, wenye walirudia mu Yerusalema, kisha utumwa wao, iliitwa Aramaiki. Walisikia sikitiko mingi, kwani pa hile fasi waliishi, hawakukuwa hekalu yao. Lakini, kwani walipenda kumuabudu Mungu wao, walisanyikwa karibu ya ma Nabii wao ao ndani ya ma nyumba iliyoitwa Sinagogi. Vile hawa watu wa Yuda walichunga dini yao mpaka hile wakati, kisha miaka 70, walirudia mu jini yao Yerusalema.

## 9. Mwisho ya utumwa

Ku mwaka 538, mbele ya uzalio ya Kristu, mataifa wa Midia na Persia walibamba muji Babilona. Chini ya hile utumwa upya taifa wa Yuda walishi na ukimya. Wakati alitawala mufalme Kiros, amri yake wa kwanza ulikuwa taifa ya Wa Yuda warudie ku inchi yao Palestina na pale wajenga Hekalu yao.

Watu wa Yuda walisikia furaha mnene. Lakini hawakupende kurudia wote, kwani watu wingi waliisha kuzaliwa pa hii muji Babilona. Ma padri na Kabila wa Levii yao na wakubwa na ma kabila Yuda na Beniamini walikamata mpango kw akurudia kwao. Mukubwa wao walimuchakula mtu moija na jina yake Zorobabeli. Huyu alikuwa toka kizazi ya Daudi na alikuwa babu ya Yosefu na Mzazi-Mungu. na taifa ya muji Babilona waliwapatia vitu vingi na makuta juu ya kujenga kasina yao. Mufalme ya Babilona Kiros alimupatia kwa Zorobabeli 5500 ma chungu takatifu, hile aliiba zamani mfalme Nebukadneza toka hekalu yao ya Yerusalema. Furaha yao hakuna namna kuiandika sisi, wakati walitembea pa udongo ya inchi yao. Mahasa ya furaha yao tunaweza kusikia, kama tutasoma ma shairi kidogo ya zaburi 126:

Wakati Bwana alipogeuza tena utumwa wa Sayuni, tulikuwa kama wenye kuota ndoto. Halafu kinywa chetu kilijazwa kucheka na ulimi wetu kuimba; Halafu wakasema katikati ya mataifa, Bwana amewafanyia maneno makubwa. Bwana ametufanyia maneno makubwa; ; kwa hivi tunafurahi. Geuza tena utumwa wetu, ee Bwana, kama mito kwa kusini. Wenye kupanda kwa machozi watavuna kwa furaha. Hata akikwenda zake akitoa machozi, akichukua mbegu za kupanda, atakuja tena kwa kelele za furaha, akileta miganda yake.

Hile wakati walianza kurima ma shamba wao. Mukubwa yao alikuwa Zorobabeli na mukubwa ya dini yao Kuhani Yesua. Kazi yao wa kwanza ulikuwa majengo ya kanisa yao. Walishangilia siku Kuu yao ilioitwa Skinopigia na ku mwaka 535 ilianza majengo ya kanisa yao na iliisha ku mwaka 516, lakini huu kanisa haikukuwa hata mkubwa na uzuri sawa hile wa zamani, iliyojenga Solomono.

Ninyi wote walibakia mu Babilona, walijizambala ma fasi ya kuachana na walifanya ma Mkini yao.

Ilipita wakati ya miaka 80 tangu hile mwaka walirudia wa Yuda toka Babilona na walirudia na ma jamaa ingine 1500, kwa mamlaka ya mukubwa yao aliyeitwa Ezdras. Walifika mu Yerusalema mu tarehe 458, mbele ya uzalio ya Kristu. Ezdras pamoja na mukubwa ya inchi yao aliyeitwa Neemia walikombana kutengeneza ma mambo yote ya taifa yao. Walikataza ma ndoa katikati ya watu wa Yuda na walio sanamu. Lakini mukana ya Kuhani mukubwa yao, jina yake Manasis, hasikutii na hasikufukuze bibi yake, aliyekuwa mtoto ya mkubwa moja toka Persia. Yeye alienda mu mji Samaria, alijenga kanisa ingine pa kilima Garizini na hivi ilikomesha hile chuki ilikuwa katikati ya watu wa Yuda na wa Samaria.

Mukubwa Ezdras alihaburu taifa yake wasome mu Sinagogi yao Sheria ya Mungu. Tena alifanya na usanyiko moja na ma Kitabu yote ya Agano la kale na hii kitabu iliitwa Kanuni ya Agano la Kale. Ku Mwisho Ezdras aliita taifa yake yote shangilio moja na aliwahubiri. Watu wote walimulaka ya kama watafata ma amri ya Mungu.

## 10. Inchi Palestina mu utumwa ya wa Grekii

Taifa ya wa Yuda walibaki chini ya utumwa ya wakubwa wa Persia miaka 200. Wakati mufalme ya Makedonia wa Grekia, aliyeitwa Aleksandros ku mwisho ya mwaka 331 alifanya nvita kupingana ya inchi Persia na alikamata muji Damaskos na Tiros, alituma makusanyo ya watu wake mu muji Yerusalema na aliomba utumwa. Kuhani mkubwa ya dini yao alikataa.

Mufalme Aleksandros alifika kisha wakati kidogo inje ya kibabashi ya Yerusalema. Taifa wa Yuda walimupokelea inje ya muji yao na mapendo. Mfalme Aleksandros kwa ajili ya hile mapokeo yao alifurahi sana. Alitembea Hekaluni yao na alitoa sadaka kwa Mungu. Alionyesha mapendo kwao na wale walimusaidia na askari mengi mu nvita yake.

Kisha lufu ya mfalme Aleksandros, inchi ya Yudea ilikuja waakati ingine pa mikono ya kizazi ya Ptolemei ya Misiri na wakati ingine pa mikono ya mamlaka ya kizazi wa Selefkides ya inchi Siria. Kisha lufu ya mufalme Aleksandos mara moja Yudea ilikuja pa mamlaka ya wa Ptolemei ya miaka 100, na wenye waliwalinzi muzuri.

Ku muji Aleksandria ya Msri walikuja watu wa Yudea wingi na walitumika na bihashara. Walifanya ma ibada yao dini yao bila mambo na walisuburia lugha kigreki, kwani tangu muda ya mfalme Aleknsandros wale watu walikuwa pa mamlaka yake walifunda na walisuburia pamoja na lugha yao na lugha kigreki. Kwa ajili ya wale wa Yudea, wenye hakujue lugha yao kiebrania, mufalme ya Msri Ptolemeos wa pili, alihamuru kundi moja ya watu makumi saba, wenye walijua ma lugha kiebrania na kigreki kufasiri Agano la Kale toka lugha kiebrania mu lugha kigreki.

Wale watu wenye hekima toka kizazi ya Yudea walitumika na walitupatia Agano la kale na fundisho yote mu lugha kigreki na kisha toka hii lugha walibeba na ma lugha ingine hii Hadisi ya taifa wa Israeli. katika hii ufasiri walifamia Fundisho wa kweli ya Mungu na wapagano na wa greki na hivi ilikuwa tayari dunia nzima kwa kufika Mwokozi yake Yesu Kristu.

Mu tarehe 198 mbele ya uzalio ya Kristu inchi Yudea ilibakia chini ya mamlaka ya kizazi wa Selefkide ya inchi Siria. Ku mwanzo uzima yao ilikuwa nzuri na watu wa Yudea wingi waliikaa mujini Antiokhia, muji kubwa ya Siria na walitumika nzuri.

Kisha wakati fulani wakubwa ya Siria waliomba palata mingi ya watu wa Yudea na jabo ingine kuliko kibaya ilikuwa hii: Mufalme yao jina yake Selefkos wa inne alikamata mpango kuiba ma zahabu na vitu vyote ya Hekalu ya watu wa Yudea. Kwa hivi alituma mkubwa wake aliyeitwa Iliodoros aingie Hekaluni. Lakini hasikuweze kufanya kintu, kwa sababu malaika ya Mungu alishuka Hekaluni, alimupiga na alimufanyisia kilonda. Yeye alianguka chini na aliruda kwa mufalme wake, bila kuiba vitu ya Kanisa.

Kisha wakubwa ya Siria walikamata mpango kugeuza mu dini yao wa sanamu na taifa ya wa Yuda. Watu wa Yude wingi walifanyika wapagano. Watu wengine waliteswa na walikufa na mateso wingi na ku mwsiho wengine walifanya nvita kupingana ya mfalme na inchi yake.

## 11. Jamaa wa Makabehi

Katikati ya wale watu walikufa katika mateso nyingi hile wakati ya wafalme ya Selefkides alikuwa na Eleazaro muzee na watoto wa saba wa Makabehi pamoja na mama wao solomoni.

Huyu Eleazaro alikuwa mwaminifu mu dini ya wa Ebrania. Wakubwa ya inchi walimusukuma akule nyama ya nguruwe, lakini hii nyama Sheria ya Musa iliikataza. Kama

muzee Eleazaro alitaka kula hii nyama hii kazi ilionyesha ya kama yeye anakataa dini yake. Walimupeleka pa fasi ya mateso yake, pahali yeye aliendа na furaha mingi. Pa njia watu ya mufalme walimushauria akule nyama ingine na atasema ya kama alikula nyama ya sadaka ya wapagano, lakini Eleazaro aliwaambia: «Haipaswe kudanyanya kwa hii kipimo uzee yangu juu ya kuokoa uzima yangu. Kama nitatoka ya apizo ya watu, kisha nitaogonjea apizo ya Mungu Mweyezi mu uzima ingine wa milele».

Hile saa ya mateso yake alisemaka: «Paka mwili yangu inateswa; lakini roh yangu anasikia furaha, kwani ninateswa kwa heshima mbele ya amri ya Mungu». HIvi huyu muzee alikufa.

Mfano ya sadaka yenye ajabu, kwa ajili ya Jina ya Munfgu Mwenyezi hile wakati ilikuwa mateso na lufu ya watoto wa saba. Askari ya mufalme waliwabamba pamoja na mama yao Solomoni na waliwapeleka mbele ya mfalme. Mfalme Antiokhos alikombana kuwakokota mu dinia ya masanamu na namna mingi na kwa kuwapiga. Hule saa ndugu mkubwa katikati yao alimujibu: «Ee mtu mubaya kabisa katikati ya watu wengine ya dunia, weye unakata hii uzima yetu, lakini Mufalme ya mbingu atatufufuka mu uzima mupya na wa milele».

Watoto wote walivumilia hii mateso yao yote. Wakati ilikuja mustari kwa kuuwa na mtoto mudogo, mufalme alisema kwa mama yake aseme kwa hule mtoto akataze imani yao na afate imani ya pagano. Hile saa mama yao mwaminifu Solomoni alisema kwa mtoto yake: «Mtoto wangu, angalia  ku mbinguni na inchi. Mungu aliumba bile bintu ni duniani hapa na watu. Usiogope hule askari. Inapaswa kusimama bila woga na pamoja na ndugu wako ingia mu uzima wa milele». Hile saa mtoto kijana alisema kwa wa askari: «Munaongojea nini? Misifata ma amri ya mufalme wenu, lakini nitafata Sheria ya Musa, Nabii wetu».

Ku mwisho alikufa katika mateso nyingi na hule kijana wa mwisho na kisha saa kidogo na mama wao Solomoni.

Kanisa yetu inashangilia makumbusho yao mu tarehe ya siku mwanzo ya mwezi Augusti ya kila mwaka.

Watu wa Yudea wengine, sawa vile tulisema, walifanya nvita kupingana ya wafalme Selefkides. Alama ya hile nvita alipatia muzee padri Matathias ku mwaka 167, mbele ya uzalio ya Kristu. Huyu pamoja na watoto wake wa tano alisirika kwa ajili ya hile mateso waliishi chini ya utumwa ya wafalme na walirudia mu inchi yao Modeini.

Toka hii fasi walienda pa milima na aliita na watu wengine wenye walitaka kumufuata. Walikuja kwao na watu wengine na hivi ilianza nvita. Kisha wakati kidogo padri Matathias alikufa na mkubwa ya hile nvita walichakula mtoto yake wa tatu, aliyeitwa Yuda wa Makaveos. Na kwa ajili ya jina yake watoto wote ya hii jamaa yao waliitwa wa Makabehi.

Huyu alishinda mara mingi ma askari ya mufalme. Mbele yab kila nvita wa askari ya Yudea walifanya sala na kifungo ya chakula. Ndani ya miaka wa wili Yudas mkubwa yao alikamata muji Yerosolima. Kazi yake wa kwanza ilikuwa matengenezo ya Kanisa yao. Alishangilia pamoja na wa ndugu wake fungulio ya kanisa yao na alijenga na kimbabasi pembeni ya Kanisa yao kwa kuilinda toka ma adui.

Kisha lufu utukufu ya Yuda pa fasi ya nvita waliendela nvita wa ndugu wake.

Hile wakati ilionekana na ma kundi ya dini wa wili. Waliitwa Kundi wa Farisayo na wa Sadukayo. Ku mwanzo wa Farisayo walikuwa watu wazuri, lakini pole-pole waliepuka toka amri wao na walifika pa hii fasi kusadiki ya kama weko watakatifu. Walifata Sheria ya Musa bila roho yao paka na namna udanganyifu. Kundi ya wa Sadukayo walikataa kwa uzima ya milele na ufufuo ya wafu. Walikataa tena Kundi ya Malaika na Maaguzi Takatifu ya Mungu.

Tena ilikuwa na Kundi wa Esehi. Hawa walikuwa watawa. Walifanya uzima ukali, lakini kosa yao ilikuwa ya kama wlaiomba mbele ya Jua, sawa mungu yao, na walifata na mafundisho ingine mapya.

Hivi pole-pole dini yao ilianguka sana. Hii ma Kundi waliikuwa na chuki katikati yao. Hali ya inchi yao ilikuwa kibaya na kizazi ya wakubwa wa Makabehi ilitembea ku mwisho yake. Wafwasi ya mwisho ya wa makabehi walikuwa Yoane Irkanoswa pili na Aristovulos wa pili.

Katikati yao ilianza nvita kwa ajili nani atakamata cheo ya Kuhani mkubwa ya dini yao. Hawa ku mwisho, kwani haikukuwe masikilizano katikati yao, waliita sawa mwenye amani yao, mukubwa Jemadari wa Roma, jina yake Pobiyo. Huyu na ma askari wake alitembea mu Palestina na aliibamba ku mwaka 63, mbele ya uzalio ya Kristu na hivi Yudea iliingia kwa utumwa ya ufalme ya Roma.

## 12. Palestina chini ya utumwa ya mamlaka wa Roma

Wakati Jemadari wa Roma Pobiyos alikamata inchi Palestina, mamlaka ya inchi alimupatia kwa Antipatros, aliyekuwa mtu wa Yudea, lakini mutu mubaya na muharibifu. Kisha miaka kidogo mwana wake Herodi alikuwa mufalme ya taifa wa Yuda na aliuwa hawa watu walikuwa jirani na wa ndugu ya kizazi ya Wamakabehi. Tena aliuwa na bibi yake, kwani na yeye alikuwa toka kizazi ya wa makabehi. Taifa ya wa Yuda walimuchukia Herodi. Huyu ni hule Herodi, aliyetafuta kuuwa na Bwana Yesu Kristu, wakati wenye akili wa tatu, wenye walikuja toka Persia, walimujulisha , ya kama walikuja kubusu Mufalme ya Yudea. Huyu tena aliuwa na watoto ya Yudea na Palestina muzima, ma elfu kumi na inne (14. 000), kwani alizania ya kama hivi ataua na Bwana Yesu Kristu.

Huyu Herodi alichakula na alisimamisha watu ya inchi yake katika akili yake na kabisa alichakula watu wenzake. Aliharabish makutano ya Wayuda na alitaka muji Yerosolima kuifanyisia muji wa zambi na kila furaha ya bure. Chuki ya taifa yake ilikuwa mingi, kwani Herodi aliweka alama moja ya ufalme wa Roma yulu ya kibabashi ya kanisa yao.

Mwisho ya Herodi ilikuwa mubaya sana. Alioza muzima. Bilulu, hile wakati yeye aliishi, walikula mwili yake. Ufalme wake, kisha aliikabula kwa wana wake wa tatu: Antipas, Filipo na Arkelao.

Hile wakati muji Yerosolima ilikuwa muji ya zambi. watu wadogo sana walikuwa waaminifu mu dinia yao na waliongolea mafikisho ya Bwana Yesu Kristu. Ni mambo ya sikitiko ya kama watu wingi kabisa waliongolea Kristu sawa mfalme moja wa hii dunia. Walimuongolea sawa mkubwa wao juu ya kufukuza mamlaka ya wa Roma na kujenga mara ingine ufalme wa Yudea, sawa zamani ilikuwa mu wakati ya mfalme Daudi. Hivi watu wingi kabisa walimuongolea Kristu.

Kwa ajili ya hii mawazo yao, wakati alikuja Kristu katikati yao, hawa watu walikataa kumufuata na kumusadiki sawa mwokozi yao toka uwezo ya shetani. Na mpaka sasa hawa watu wa Izraeli hawasadiki Bwana Yesu Kristu sawa Mwokozi ya dunia muzima toka zambi na mamlaka ya shetani.

Sisi sawa vile tunajua Yesu Kristu alikuja mwenye amani, mupole na munyenyekevu, hile wakati mu Palestina na Yerosolima hali ilikuwa mubaya sana.

# KIPINDI CHA SITA

## UFUNUO YA MUNGU NA KATIKA WATU WESHIMIWA WENGINE

### `1. YOVU

Mu inchi Afsitis aliishi mtu moja aliyeitwa Yovu. Huyu alikuwa mutu wa kweli, musiyekosa, mwenye haki, mweshimiwa  na bila kufanya matendo maovu, sawa vile inatwaambia na Madiko Takatifu. Yeye alikuwa na watoto wa kumi, wanaume saba na wanawake  tatu, ma nyma mengi na mali mingi. Alikuwa mutu mwenye heri na kila siku alimutukuza Mungu.

Lakini hii furaha na mali yake chetani aliichukia. Alibeba baraka toka Mungu juu ya kutesa mutumishi yake Yovu. Mungu alimupatia ruhusa na shetani alianza hivi kumupima mfano na ma fazila yake.

Siku moja, wakati Yovu aliikaa wa furaha mingi, alikuja mutumishi yake moja na alimwambia:

-Walikuja watu wabaya na waliiba ma ngombe na ma punda na waliua watumishi wote wetu. Paka mimi niliokolewa na nilikuja kwako kukuwambia hii mambo.

Kisha saa kidogo mutumishi mwingine alikuja kwa mkubwa Yovu na alimwambia:

-Toka mbingu ilianguka moto na ma kondoo na wachungazji wote iliwalungua. Paka mimi niliokolewa na nikuja kwako kukuwambie hii mambo.

Tena hile saa mutumishi mwingine alipaza sauti:

Watu wanyangani waliiba ma ngami wetu na waliua watumishi wetu.

Na mutumishi wa inne alikua hii saa kwa kumujulisha mateso ingine:

-Mkubwa wangu Yovu, watoto na wa binti wako wote walikuwa nyumbani ya ndugu wao mkubwa. Lakini mara moja pepo nguvu ilifanyika na ufuniko ya nyumba yao ilibomoa na watu wote walikufa ndani ya hile nyumba.

Yovu alilamuka na alipasuka mupila yake kwa ajili ya sikitiko wake, katika kutim ya hile wakati. Alikata ma nywele yake yote toka kichwa yake, kisha alipika magoti mbele ya Mungu na alimwambia hivi: «Mimi, ee Bwana, nilizaliwa mutupu toka tumbo ya mama yangu na nitatoka pale paka hivi. Wewe Bwana ulinipatia, Wewe ulinitosha. Ilifanyika katika mapenzi Yako. Jina

ya Bwana ni ubarikiwa wa milele».

Wakati shetani aliona ya kama hii mateso mengi hakuna namna kuharabisha imani nas uvumilia ya Yovu, aliomba mara ingine toka Mungu kumuuzi Yovu pa mwili yake. Mungu, juu ya kuonekana kuliko nzuri, imani ya Yovu, alimupatia kwa shetani ruhusa Wake. Paka, uzima yake haipaswe kuiuzi.

Vilonda wingi walijaza mwili yake na maumivi nyingi walimuteswa. Yuvo alisimama yeye wa pekee inje ya muji na alikulula ma vilonda wake. Pembeni ya hii mateso yake alikuja na bibi yake na alimuchabula hivi:

Mupaka wakati gani utafanya uvumilia? Ulipotesha vitu vyako vyote na watoto na mali na urtukufu na sifa ya jina yako. Basi, umuchabula Mungu na kisha, kufa. Lakini Yovu alimujibu hivi kwa bibi yake:

-Juu ya nini ulisema hivi sawa moja mwanamuke asiye na akili? Kama mali na vitu yote Mungu aliitupatia, sasa tutakataa kuvumilia kila mateso hile Mungu anaitupatia?

Hile wakati wafalme tatu, wenye waliikaa pembeni ya inchi ya Yovu, wakati walisikia mateso yake, walikuja kwake na walimubembelesha. Wakati waliona mateso yake, walibakia ma siku saba, bila kusema sauti moja kwa ajabu yao. Ku mwisho Yovu alifungula Yovu kinywa yake na alifiga hile siku yeye alizaliwa. Ndugu wake walimwambia yakama kwa ajili ya zambi yake alipata mateso mengi na Mungu alisirika kwake. Lakini Yovu aliwaambia ya kama hasikufanye zambi mbele ya Mungu , lakini ma rafiki yake walimutia mtu mwenye zambi.

Hil; e wakati alikuja Mungu katikati ya mawingu na aliwaambia ya kama watu hana na ruhusa kuzungumuza na kuhukumu mawazo ya Mungu, kwani hawaweze kusikia akili Yake. Paka Mungu anajua faida ya roho ya kila mtu na anatengeneza uzima na wokovu ya kila mtu katika mapenzi yake takatifu. Kisha ma sauti ya Mungu Yovu alitubu, kwa sababu alilaana hile siku alizaliwa, lakini na rafiki wake walitubu, kwani walimuita mtu mwenye zambi. Na Mungu, kwani aliona uvumilia ya Yovu, alimutunza ya ugonjwa wake, alimupatia watoto wengine na wa binti na ma kunzdi ya ma nyama na vitu vyote kuliko mengi ya zamani.

Vile aliishi Yovu miaka mengi na alikufa mu kipimo uzee. Kwa ajili ya ma fazila yake Kanisa ya Kristu alimusifu sawa mtakatifu na mwenye haki na alishangilia ukumbusho yake mu tarehe 6 Mwezi ya Tano.

Basi, na sisi inapaswa kuvumilia kila mateso na taabu yetu. Sawa vile zahabu inasafishwa ndani ya moto, vile na kila mtu anatakaswa katikati ya ma taabu na mateso ya hii uzima.

## <u>2. Vijana wa tatu ndani ya tanuru</u>

Katika mwaka 586, mbele ya uzalio ya Kristu, mfalme ya muji Babilona jina yake Nebukadneza wa pili alikamata Yerosolima. Mufalme alikamata na watu wingi na aliwapeleka mujini Babilona sawa watumwa. Watu wa Yuda waliishi mu inchi ugeni miaka 70. Mufalme alisema kwa wakubwa wake kwa kuchakula vijana wazuri katikati ya kabila ya taifa wa Yuda juu ya kufanya kazi ya inchi yake. Basi walichakula vijana wa tatu: Hanania, Misaeli na Azaria, ambayo waliwapatia jina ya lugha yao. Hivi Hanania-Sadiraki, Misaeli-Mesaki na Azaria-Abedenego Tena mfalme alihamuru wale vijana kuvaa manguo mapya na mazuri na watakula pamoja naye. Lakini hawa vijana walikuwa waaminifu mu dini yao na hawakukule kila chakula, kwani dini yao iliwakataza. Walikula paka mahalaki na walikunywa maji. Kwa ajli ya heshima yao Mungu aliwabariki na miili yao ilikuwa nguvu. Tena na imani yao kwa Dini ya Wapateri wao iliwapatia nguvu kuliko mingi. Ilifika sasa wakati moja na hawa vijana walionyesha nguvu ya imani yao.

Mfalme siku moja alifanya picha moja na uso yake na zahabu. Alituma watumishi wake pa fasi yoyote ya inchi yake juu ya kujulisha kwa watu wote wafika siku fulani kwa shangilio ya hii picha ya uso yake. Walikuja hile siku watu ya taifa yake na ilipaswa kusujudu na kubusu sawa mungu picha yake. Kama mtu moja atakataa kusujudu na kubusu uso yake, watamuweka ndani

ya moto akufe.

Walikuja na hawa vijana wa Yuda, lakini wale waliabudu paka Mungu ya kwelina walikataa kubusu sawa mungu picha ya mufalme yao. Waakti alisikia hii mambo mfalme aliwaambia kusimama mbele yake. Na sasa hawa vijana hawakupotesha nguvu na imani yao. Mufalme aliwaambia kwa kumuogopa ya kama ataanza kuwafanysia mateso nyingi. Hawa vijana walimwambia: Ni Mungu wetu wa mbingu na Huyu sisi tunamuabudu. Yeye ni Mwenyezi na anaweza tuokoe toka hii tanuru ya moto».

Hile saa mfalme alihamuru kuweka moto kuliko mingi ndani ya hii tanuru na ndani yake watatupa hawa watoto. Amuri yake ilitimizwa. Lakini ilifanyika mambo moja wa ajabu. Ndani ya tanuru walisikia wimbo utamu na hapana ma taabu na malalamiko. waakti walikaribia wa askari ya mfalme waliona hawa vijana bila monyororo pa mikono yao; waliimba wimbo vizuri na waliomba kwa Mungu. Katikati yao alisimama na Kijana mwingine, aliyekuwa na uso uzuri sawa malaika ya Mungu.

Na kweli huyu alikuwa Malaika ya Mungu, mwenye aliharabisha nguvu ya moto na watoto walisikia baridi. Mbele ya hii muujiza wa ajabu mufalme alitubu na alihamuru kutosha inje hawa Vijana, bila kilonda hata mambo mu miili yao.

Hile saa mfalme alipaza sauti: «Mungu ya Hanania, Misaeli na Azaria ni mubarikiwa, mwenye alituma Malaika wake na alitosha watoto wake wasiyo kilonda kidogo». Kisha mfalme alituma amri yake mu inchi yake yote na aliwaambia watu kuheshimiwa wote Huyu Mungu ya wale watoto , kwani YEYE ni mkubwa na Mwenyezi, «Ufalme wake ni wa milele na mamlaka wake kwa kizazi na kizazi».

Wakati hawa Vijana walikuwa ndani ya tanuru ya moto waliimba hii wimbo mbele ya Mungu:

Enyi nyote, viumbe vya Bwana, mkuzeni Bwana, kwake utukufu mkuu na sifa milele.

Enyi nyote, Malaika wa Bwana, mbingu za bwana, mkuzeni Bwana, kwake utukufu mkuu na sifa milele.

Enyi maji ya juu ya anga, mawazo yote ya Bwana, mkuzeni Bwana, kwake. . .

Enyi jua na mwezi, nyota za mbinguni, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Enyi nyote, mvua na mawingu, enyi nyote pepo, mkuzeni Bwana, kwake. . .

Enyi moto na hari, kipwa na masika, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Enyi umande na sakitu, gandamizi na baridi, mkuzeni Bwana, kwake. . .

Enyi barafu na seluji, usiku na muchana, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Enyi mwanga na giza, umeme na mawingu, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Enyi milima na vilima, mimea yote mchipukayo katika inchi, mkuzeni Bwana, kwake. . .

Enyi chemchemi, bahari na mito, nyangumi na vyote vitembeavyo majini, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Enyi nyote ndege za angani, nyota wanyama wa porini na mifugo, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Enyi wanadamu, ewe nyumba ya Israeli, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Enyi Makuhani, watumishi wake, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Enyi mioyo na roho za watu wema, enyi Watakatifu na wanyenyekevu wa moyo, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Hanania, Azaria, Mishaeli, mkuzeni Bwana, kwake utukufu mkuu na sifa milele.

Mitume, Nabii ma Mashahidi wa Bwana mkuzeni Bwana. . .

Tunamsifu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Bwana tunamuhimidi na tunamutukuza milele na milele.

Tunamsifu, tunamuhimidi na tunamsujudu Bwana.

Bwana tunamuhimidi na tunamutukuza kwa milele wote.

## 3. Esiteri

Katikati ya wale watu walitembea mu utumwea mu inchi Persia walikuwa na Mordekayi na mwipwa yake binti Esiteri. Huyu mwaname alionyesha kwa mufalme ya Persia jina yake Ahasuero imani, mapendo na utii yake. Huyu Mordekayi zamani aliokoa mufalme kwa sababu alimwambia mawazo mabaya ya watu wa wili wake, wenye walitaka kumuua mufalme Ahasuero. Hii tendi nzuri yake watu ya mfalme waliiandika pa vitabu ya inchi yake.

Hile wakati bibi ya mfalme jina yake Astini, alifanya kosa moja, kwani alikataa kutii amri ya bwana wake. Kisha mufalme alimufukuza, kwa sababu mfano yake ilikuwa mubaya mbele ya wanawake nyingine ya inchi yake na alitafuta bibi mwingine. Basi, siku moja walikuja Nyumbvani kubwa ya mfalme wanawake vijana nyingi na katikati yao alikuwa na binti moja ya kabila wa Yudea, jina yake Esiteri. Huyu alikuwa mtu muzuri, mupole na mwenye akili. Huyu alimuchakula mufalme ya bibi yake.

Esiteri aliingia Nyumbani kubwa ya mufalme. Pale muyomba yake Mordekayi alimutembelea na alimushauria. Tena alimwambia kufuchama ya kama ni toka kabila ya waYuda, dini yao na ya kama ni mwipwa yake.

Kisha mwaka moja mufalme alimupatia taji Esiteri na alimwita bibi yake. Na Esiteri alipata utukufu mnene, lakini hasikusahau kizazi na Kabila yake. Alionyesha hii mapendo yake, wakati watu wa Yuda walipata hatari moja mnene.

Mtu moja aliyeishi katikati ya watumishi ya mufalme jina yake Amani alikombana na namna ukalamushi alimulanda mufalme na alipanda ma cheo yulu kabisa ndani ya ufalme wake. Hata mnene ilikuwa utukufu ya bure yake mpaka alifika kumwambia kwa mufalme atume barua yake mu taifa ya inchi yake yote na watu wote kumusujudu Amani sawa mungu wao.

PakaMordekayi, alibakia mwaminifu pa amri ya Mungu: Utasujudu paka Bwana Mungu wako na paka Huyu utamuabudu». Na alikataa kumusujudu Amani.

Wakati alisikia hii jabo Amani alisirika na alitafuta namna gani atamuua Mordekayi na watu wa Yuda wote.

ya kwanza aliwaza kusema sauti ya wogo kwa mufalme juu ya kuandika barua moja kwa kuua watu wa Yuda wote. Basi, aliwasitake ya kama hawatii kwa amri ya mfalme na wanapatia mfano mubaya mbele ya watu wengine ya inchi yao. Vile mufalme alisirika na aliichika kuandika barua moja na tena alisema na siku gani watu wa Yuda wote watakufa.

Wakati alijulia hii mambo wa sikitiko mingi Mordekayi alipasuka manguo yake, aliweka pa kichwa yake maivi katika kutim yao na aliikaa na taabu mingi inje ya nyumba ya mufalme. Alimwambia na kwa bibi ya mufalme, mwipwa yake Esiteri juu ya hii mateso itafika kwa mikono ya bwana wake. Esiteri alipenda wa ndugu wake. Alisikia na aliona sikitiko ya muyomba yake na aliwaambia ndugu ya Kabila wake kufanya sala na imani nguvu kwa Mungu na kifungo ya chakula.

na huyu Esiteri alifanya sala ma siku tatu. Kisha alisimama mbele ya bwana yake mufalme ya Persia na alimwambia kufika huyu pamoja na mkubwa Amani mu chumba yake juu ya kula pamoja. Mufalme bwana yake aliichika na furaha.

Hile usiku mufalme hasikuweze kupumzika na lisema kwa musaidizi yake kusoma toka hii Kitabu ya ma tangazo ya ufalme wake. Waakti msomaji alifika pa hii fasi waliandika ya kama huyu mugeni Mordekayi alimuokoa mufalme kwa ajili ya watu wa wili, wenye walitaka kumuua fufalme, huyu aliuliza: «Malipo nini tulimupatia kwa huyu mugeni, mwenye aliniokoa zamani? Watumishi wake walimwambia ya kama hata malipo na cheo moja hawakumupatie.

Hile saa mufalme alitafuta majulisho ya Mordekayi, mara moja alikuja ndani na mkubwa Amani. Mufalme alimuita na alimuuliza:

-Ee Amani, uniambie, kama mufalme anataka kusifu mutu moja inapawa kufanya nini?

Amani aliwaza ya kama ni huyu, mwenye mufalme anataka kumusifu. Joo hivi alisema kwa mufalme:

-Huyu mutu inapaswa kuwa na mavazi mazuri sana, kuikaa pa punda ya mufalme, kuwa moja mkubwa ya ufalme ya mufalme na kutembea pa punda katikati ya njia na kusema: Tazama, namna gani mufalme anasifu wandugu wapenzi wake.. .

-Shauria yako ni nzuri, alimujibu mfalme. Basi, ninakupatia amri yangu kuvaa hivi hule mugeno wa Yuda Mordekayi na utamutembelea pa punda katikati ya njia ya muji yetu na weye utakokota na kamba punda yake. Hii amri hapa sana ninataka kuitimiza.

Amani alisituka, wakati alisikia amri ya mfalme. Inapaswa kutii juu hapana kupotesha kichwa chake.

Lakini Mungu aliisha kutengeneza na ingine apizo mnene kabisa kwa hule Amani.

Mufalme alifurahi sana kwa ajili ya vile vitu ya chakula alitayarisha bibi yake na alimulaka ya kama atamupatia kila kintu bibi yake atamuomba, hata na kipande moja ya ufalme wake.

Hile saa Esiteri alifungula roho yake mbele ya mfalme bwana yake na alimwambia ya kama ni toka kabila ya wa Yuda na ya kama akbila yake ni mu hatari mnene kwa ajili ya mutumishi yake Amani, mwenye anataka kuharabisha kabila yake. Mufalme, bwana yake alisikia hiiudanganyifu na ukafiri ya Amani. Alihamuru wa askari wake, walimubamba na walimutundika pa hile kamba aliisha kuitayarisha Amani juu ya kutundika Mordekayi. Tena mufalme alizimisha amri yake juu ya kuua Kabila ya wa Yuda na alimwita Mordekayi na alimupatia cheo hile alikuwa mpaka hile siku adui yake Amani.

Vile Mungu aliripa Mordekayi mwaminifu yake na alipiza matendo mabaya.

## <u>4. Yudithi</u>

Ku mwaka 350 mbele ya uzalio ya Kristu taifa wa Persia walikamata ufalme ya Izraeli na kisha walikombana kukamata na ufalme ingine iliyoitwa wa Yuda.

Jemadari mkubwa wa inchi Persia ya kundi ya askari alikuwa mtu moja jina yake Oloferni. Huyu na amri ya mufalme wake aliingia ndani ya inchi ya ufalme ya Yuda pamoja na askari wake. Aliharabisha kabisa ma muji na mukini wao na alirima ma fasi yote lufu na uharibifu.

Watu wa Yudea walisituka, waliogopoa na walifanya nguvu kujenga kiibabashi pembeni ya muji yao. Taifa yao walivaa manguo ya taabu na walilia sana na waliomba kwa Mungu awaokoe.

Na huyu mkuwa ya dini yao Kuhani Yoakimu alizunguluka katikati ya ma muji yao na aliwashauria wote kumuomba kwa Mungu. Aliwaambia ya kama Mungu atawaokoa mara moja, sawa na zamani. Na sasa katika sala na imani yetu tutaokolewa, aliwaambia waaminifu wake.

Vile aliandika na kwa watu ya muji Vetilua, pahali watu walikombana kufunga hile njia ya kupitisha Oloferni na kundi ya askari yake. Oloferni alifika pa hii muji lakini hasikuweze kuibamba, kwani watu yake waliichunga nguvu. Juu ya kusukuma watu ya hile muji kutoka, Oloferni alikata pombi ya maji ya muji yao. watu wingin ndani, kabisa wanawake na watoto, walikufa kwa ajili ya kihu, na weingine walibakia na kidogo nguvu, walikamata mpango kujitoa.

Hile wakati ya hatari alikuja katikati yao binti moja muzuri, aliyependa inchi yake na alikuwa na mweshimiwa. Huyu alikuwa bibi ya Manasis, aliyekufa zamani. Huyu Yudithi alisema mbele ya wakubwa ya inchi yake:

Ee Wakubwa, haipaswe kuijitoa muji yetu kwa adui wetu. Mungu wetu, mwenye alituokoa zamani ya kila hatari, kama tunamuamini nguvu, anaweza na sasa atuokoe.

Sauti yake aliwapatia nguvu kwa wakubwa. Kisha Yudithu aliendelesha sauti yake:

-Mweye mukombane kuchunga na ma nguvu yenu yote muji yetu. Mimi nitaingia mu fasi ya wa adui na nitatafuta kukutana na jemadari Oloferni.

Vile alisema Yudothi na wote waliichika. Huyu mwanamuke ya kwanza aliomba kwa Mungu amusaidie na aokoe inchi yake. Usiku moja pamoja na musaidizi mwanamuke moja walitoka ya fasi yao na walitembea mu fasi ya kundi ya wa adui. Wachungaji, wenye waliwabamba, waliwakamata, lakini Yudithi alisema ya kama anaenda kukutana na mkubwa yao. Wachungaji askari walimupeleka kwake. Huyu mwanamuke alimwambia hivi:

-Ninachukia watu wa Yuda na ninataka kujiharabisha. Mimi nitakujulisha mawazo wao wa siri na hivi utakuwa mbio-mbio mkubwa ya muji Vetilua. Juu ya kusadiki ya kama mimi ninakuwambia kweli unichunge karibu yako sawa mutumwa wako.

Oloferni jemadari alisadiki sauti ya Yudithi. Alimuchunga mu fasi yake na alimuacha kutembea na uhuru katikati ya adui yake. Yudithi usiku moja, hile wakati Oloferni alilala, aliingia chumbani yake na kisu moja alikata kichwa chake. Kisha, bila mambo alitoka inje ya fasi ya adui na alitudia mu mji wake. Waakti watu wa Persia walisikia lufu ya mkubwa wao, walisimamisha nvita na walirudia kwao.

Hivi kwa ajili ya hile mapendo alionyesha Yudithi mu inchi yake, iliokowa na muji na inchi yake na wa ndugu wake waliokolewa.

## 5. Toviti

Toviti alizaliwa mu mji Thisvi ya Yudea. Alikomea pa mikono ya kambo mwanamuke wake, jina lake Devora, aliyemufundisha kuwa mwenye heshima na kufata kupasua ya dini yao.
Wakati alikomea, aliowa binti Anna na walizala mtoto moja jina lake Tovia.

Wakati mfalme wa taifa Asiria alishinda taifa ya Yudea, katikati ya watumwa, ambayo wapeleka mu muji Ninevi alikuwa na Toviti pamoja na jamaa yake. Hile wakati ya utumwa wao, watu wa Yuda wingi walisahau dini yao, lakini Toviti alibaki mwaminifu mu imani yao. Tena katika hatari ya uzima yake, alikombana kuzika maiti ya wa ndugu wake, wenye mufalme aliwaua, kwa sababu ilikuwa shewria ya dini yao hapana kuacha maiti yao inje bila maziko, lakini amri ya mufalme ya muji Ninevi ilikuwa kuacha maiti yai inje bila kuwazika.

Wakati moja mara moja Toviti alipotesha nuru ya ma macho yake. Kwani sasa alikuwa kipofu haikukuwe namna kutumika. Mambo ya uzima yao alianza kutengeneza bibi yake Anna, mwenye alianza kutumika. Lakini hii feza alibeba ya kazi yake haikukuwe mingi na hawa waliteswa. Hile wakati Toviti alikumbuka, ya kama hile wakati zamani alikuwa mutajiri, alipatia sawa deni makuta fulani kwa jirani wake Gabrieli, aliyeikaa mujini Ragi ya Media. Basi, aliita mwana wake Tovia na alimwambia aende mujini Ragi kubeba makuta yao. Kwa sababu alikuwa muzee, na aliogopa ya kama atakufa, alimupatia na ma shauria yake ya mwisho: Mtoto wangu inapaswa kusifu mama yako na usimutaabu hata kidogo. Kwa kuwa daima mwenye haki na murahimu. Chukia majivuno na penda watu wote. Kama mtu moja atakufanyisia kazi kimoja kibaya, weye usimupatie hii kazi kibaya. Kumbuka daima Mungu, umutukuze na umuombe akusaidie na hivi njia yako itakuwa nzuri». Tovia alisikia ma shauria ya baba yake na alimulaka ya kama ataichunga mu uzima yake. Aliichika aende mujini Ragi ya Media. Lakini ilipaswa kutafuta mtu moja sawa mwongozi, kwani hii muji ilikuwa mbali. Alitoka inje ya nyumba yake kutafuta mwongozi na inje ya mulango yake, alikuta mwanaume moja, aliyekuwa mutu wa ajabu. Huyu mugeni aliichika mara moja kumusindikiza Tovia mu safari yake. Huyu kijana alikuwa Malaika ya Mungu na jina yake Rafaili, mwenye alimutuma Mungu amuongoze Tovia mu safari wake.

Malaika hasikuseme nani alikuwa. Alisema paka ya kama anaitwa Azaria, mwana wa Anania na aliomba tena na malipo ya hii kazi yake.

Kisha ma siku nyingi walifika karibu ya mutoni Tigris ya Mesopotamia. Pale walisimama kidogo kupumuzika na kunawa. Wakati Tovia aliingia ku maji, samaki moja mnene alikuja kwake. Malaika alimuwambia na sauti ngivu kumubamba huu samaki na kumukokota inje ya maji. Tovia alifanya hivi. Malaika alimwambia kutosha roho na nyongo ya samaki, kwani ni sawa dawa ya wale watu walipotesha nuru ya ma macho yao.

Siku ingine walifika nyumbani ya Raguili, pahali Tovia, katika shauria ya Malaika aliowa binti ya hule mutu jina yake Sara.  Malaika Rafaili, katika sauti ya Tovia, alienda mujini Ragi ya Media na alibeba hii makuta.

Kisha walirudia na Sara mujini Ninevi, pahali walimuongojea wazazi wake. Alimumbatia Tovia baba yake na alipakaa na hii nyongo ma macho yake. Ma macho yake mara moja

ilifunguliwa. Toviti aliona mwana wake, alimubariki na alimushukuru Mungu kwa hii tunzi yake.

Kisha aliita hule mugeni juu ya kumupatia makuta yake. Lakini hule alimwambia: Mimi ni Rafaeli, Malaika moja ya Mungu na ninasikia na ninabeba ma sala ya watu na ninapeleka kwa Mungu na ninasimama mbele ya Kiti ya Mungu Mwenyezi». Mimi nilipeleka kwa Mungu ma sala na matendo yako mazuri. Hata tendo moja haikuzarau Mungu na kwa hivi Yeye alinituma kwako akutunze na akusaidie pa hii mambo na sikitiko yako».

Wakati walisikia hii sauti ya Rafaeli Toviti na mwana wake, walianguka chini kw aajili ya woga wao. Lakini Malaika alisema mara ingine: «Musiogope, amani ni katikati yenu; Mumuhimidi Mungu kwa milele.. . na muandikeni hile matendo yote ndani ya kitabu moja». Alisema hii sauti yake na alikimbia.

Toviti aliishi tena, kisha tunzo ya ma macho yake, na alifanya matendo mazuri wa mapendo na aliogopa Mungu mpaka ku mwisho ya uzima yake.

# KIPINDI CHA SABA

## 1. Manabii

Kisha lufu ya Solomono, mwana wa daudi, ufalme wa Izraeli, ilianza kuanguka. Mwanzo ya uharibifu yake ilikuwa uchanisho ya ufalme moja na walifanyika mafalme wa wili: Ufalme wa Izraeli na mufalme Roboamu, mwana wa Solomono na ufalme wa Yuda na mufalme Yeroboamu, mutumwa ya Solomono. Hile wakati ilionekana jabo mojakubwa kabaila. walikuja watu wenye walisema ma sauti katika mwangza ya Mungu. Waliitwa Manabii.

Zamani waliisha kusema vile vitu watafanyika wanaume wakubwa sawa Noa, Abrahamu, Isaaka, Yakobo, Musa, Samueli na wengine. Lakini hii wakati wanaonekana kkuliko wingin Wanabii.

Nabii anaitwa kabisa huyu mtu mwenye katika nuru ya Roho Mtakatifu na ufunuo ya Mungu, anasema vile matendo watafanyika kisha wakati ingine. lakini Manabii waliitwa na wale watu weshimiwa, wenye walifundisha taifa ya Mungu kwa kufata amuri Yake.

Nikusema tendo ya Manabii ilikuwa kufundisha dinia wa kweli, kushauria watu hapana kufata uzima ya zambi , walihubiri sauti ya toba na kusema kwa taifa ya kama Sheria ya Musa ilikuwa mwanzo ya sheria ya Mukombozi Bwana Yesu Kristu.

Manabii walihubiri ma fasi ya kuachana, inje ya lupngo ya ma kanisa ya Wayuda, inje ya ma nyumba ya wafalme na mu soko na ma fasi ingine.

Manabii ni ma vipande wa wili: Mu Kipande ya kwanza wanaitwa manabii wakubwa na mu Kipande wa pili wanaitwa Manbii Wadongo. Mwito yao ilitoka ya makitabu yao, ili waliandika. Manbii wakubwa walikuwa na Elia na mwanafunzi wake Eliseo, lakini hawa hana ndani ya ma kundi ya Manabii wakubwa ao wadogo, kwani hawakuandika ma kitabu yao. Manabii wakubwa ni hawa wafuata sasa: Isaya, Yeremia, Ezekieli na Danieli. Manabii wadongo weko kumi na mbili: Hosea, Amosi, Mika, Yoeli, Obadia, Yona, nahumu, Habakuki, Zefania, Hagai, Zekaria na malaki.

## 2. Nabii Isaya

Nabii moja mkubwa kati ya wengine alikuwa na Isaya. Aliishi miaka 800 mbele ya uzalio ya Kristu ndani ay ufalme wa Yuda. Alikuwa mtu mwenye hekima na mwenye akili. Kisha doa yake alizala watoto wa wili;

Siku moja, alikuwa karibu ya mulango ya hekalu ya Solomono na alimuona Mungu sawa ono na aliikaa pa Kiti urebu na kubwa na pembeni yake Malaika wingi waliimba hivi: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Savaothi, mbingu na inchi zimejawa kwa utukufu wako». Moja malaika alimukaribia Isaya, alisafisha midomo yake kwa kuwa safi na stahili kutumika hii kazi ya Mungu na alisema kwake:

«Mimi nitamutuma nani, na nani atakayekwenda kwa sisi? Isaya alimujibu: Mimi hapa, unitume mimi. (Malaika) akasema: Kwenda na utawaambia watu hawa: Kusikia mutasikia, lakini hamutafahamu; na kuona mutaona lakini hamutajua. Ufanyize moyo wa watu hawa kuona, na ufanyize masikio yao mazito, na ufunge macho yao; hata wasione na macho yao, na kusikia na masikio yao, na kufahamu na moyo wao, na kugeuka na kupona» (Isaya 6, 8-10).

Mungu na hii ma sauti alisemaka kwa Isaya ya kama alipaswa kuhubiri toba kwa Taifa wake na kurudia kwa Mungu wa kweli, kwani mateso nyingi itawafata, kama watakataa kutubu.

Sawa vile sisi tunajua hile wakati, ufalme ya waYuda ilipasuka na vipande wa wili, taifa wa Yuda ilitoka mbali ya dini ya Wababu wake. Watu walisadiki wa mungu wa wogo na dini yao ilibaki paka kwa kufata ma alama na ma ibada yake, bila maana na uzima ukweli..

Isaya alitaabu kwa ajili ya hii hali ya taifa yake na alizimisha kuhubiri na kurudia juu ya kurudia taifa kwa Mungu. Kwa hivi ma siku zote alisemaka:

-Mungu hasipende kumuabudu paka na midomo yenu, lakini na moyo yenu.

Pempeni ya hii hali kibaya yao, ilikuwa na matendo mbaya ingine, hile wakati ya Isaya. Wakubwa wao walikuwa wazulumu. Watu walikuwa wenye majivuno. Walipenda utukufu ya dunia na walivaa manguo na majivuno mingi.

Nabii Isaya katika hubiri yake aliwaambia mara nyingi: hakuna faida hata kidogo kwa ajili ya sadaka wenu mbele ya Mungu. Mungu hasipende mafungo ya chakula yenu, hata ma Siku Kuu wenu, kwa sababu uzima yenu ni yenye zambi. Mutubu na musafishe ma nafsi wenu na mutoshe mawazo uovu wenu. Muzombelee kufanya kazi kizuri na musaidieni wanawake wasiyo mume na watoto wa yatima. Mutubu na muungame na Mungu atamisamehe. Kama mutafanya mapenzi ya Mungu, mutaishi wenye heri. Kama musitafanye mapenzi wake, inamiongojea malipizo nyingi.

Nabii Isaya aliwaambia ya kama itafika na ma nvita nyingi na utumwa na uharibifu na hii yote ilifanyikwa kisha wakati kidogo. Tena alimushauria na mufalme na sauti yake ukali, lakini yeye hasikusikie sauti yake na mateso nyingi ilikuja mu taifa yao.

Nabii Isaya ni Nabii mkubwa kupita ya weingine wote na anaitwa tena sawa Nabii Mwevangelizaji, kwa sababu alihubiri juu ya ufikisho ya Bwana Yesu Kristu. Nikusema alisema, mbele ya kufika Mweokozi duniani, ya kama Yeye ataitwa Emanueli, ya kama Yeye atakuwa Mungu m, wenye hekima na mwenyezi, atahukumu na haki kila mtu munyenyekevu na maskini, ataokowa wenye zambi na ataopoa watumwa na ataleta amani. Ku mwisho katika Usulumbio yake ataokoa dunia toka zambi.

Isaya alikufa katika mateso nyingi ku wakati ya mfalme Manasis, mwenye, katika mapokeo, alimukata vipande-vipande mwili yake na shoka moja na hivi alikufa pole-pole. Nabii Isaya ni Mtakatgifu ya Kanisa yetu na anashangilia mu tareha 9 Mwezi ya Tano. Tazama masauti yake juu ya ufikisho ya Yesu Kristu:

**Uzalio ya Kristu toka Bikira Mzazi wake Maria:**

«Tazama Bikira atapata mimba naye atazaa mutoto mwanaume, na ataita jina lake Emanueli» (Isaya 7, 14).

**Mwokozi ni mkubwa wa salama.**

«.. . Maana kwa ajili yetu mutoto amezaliwa, tumepewa mutoto mwanamume; na utawala

utakuwa juu ya bega lake: Na jina lake litaitwa Mwenye ajabu, Mwenye shauri, Mungu Mwenye uwezo, Baba ya milele, Mukubwa wa salama. Kuongezwa kwa utawala wake na salama hakutakuwa na mwisho, juu ya kiti cha ufalme cha Daudi, na juu ya ufalme wake kuusimamisha, na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele» (Isaya 9, 6-7).

**Unabii juu ya usulubio ya Mwokozi.**

«.. . Yeye hana sura wala uzuri, na wakati tunapomwona hana uzuri hata tumutamani. Amezarauliwa na kukataliwa na watu; Mutu wa huzuni, na mwenye kujua taabu: na kama mutu watu wanayemufichia nyuso zao, alizarauliwa, na hatukumuhesabu kuwa kitu. Kweli amechukua taabu zetu, na amebeba huzuni zetu; lakini tulimwona akipigwa, akiteswa na Mungu, na kuhuzunishwa. Lakini aliumizwa kwa makosa yetu, alichubuka kwa maovu yetu. Azabu ya salama yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepotea; Tumegeuka kila mumoja kwa njia yake mwenyewe; na Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote. Alionewa, na aliteswa, lakini hakufungua kinywa chake; Kama mwana-Kondoo anayepelekwa kuchinjwa na kama kondoo anavyonyamaza mbele yao wanaokata manyonya yake; hakufungua kinywa chake. Aliondolewa kwa kuonewa na kuhukumiwa, na kwa kizazi chake, nani aliyewaza ya kuwa amekartiliwa mbali na inchi ya walio hai; alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu. Wakamufanyia kaburi pamoja na waovu; na pamopja na matajiri katika kufa kwake; hata yeye hakufanya jeuri, wala hila haikufanya kinywani mwake.. . » (Isaya 53, 2-9).

## 3. Nabii Yeremia

Nabii Yeremia ni katikati ya Manabii makubwa. Aliishi miaka miya sita mbele ya kuzaliwa Kristu, nikusema wakati ya utumwa na aliikaa mu Palestina. Yeye alikuwa na mapendo kubwa kwa inchi yake na imani kwa Mungu. Alitaka kuona taifa ya Yuda kutimiza amri ya Mungu. Mungu alimuita pa cheo ya nabii, wakati yeye alikuwa kijana. Tazama namna gani Yeremia anaandika mwito ya Mungu: «Ilipokuwa sijakuumba bado katika tumbo nilikujua na ilipokuwa hujatoka bado tumboni, nilikutakasa nimekuweka kuwa nabii lamataifa» (Yeremia 1, 5). Lakini Yeremia alimujibu Mungu: «Ee Bwana Mungu! Tazama, siwezi kusema; kwa sababu mimi ni mutoto. Lakini Bwana akaniambia: «Usiseme: Mimi ni mutoto, kwa maana utakwenda kwa kila mutu nitakayekutuma kwake, nawe utasema kila neno nitakalokuagiza. Usiogope mbele yao, kwa sababu mimi ni pamoja nawe nikuokoe, anasema Bwana» (Yeremia 1, 6-8).

Yeremia alianza mara moja kusema ma sauti ya unabii. Alisema unabii moja juu ya uharibifu ya ufalme wa Yuda na utumwa, kama malipizi ya Mungu kwa ajili ya zambi ya taifa. Aliandika ma unabii yake yote na taifa aliisoma na pasopo mingi. Alihamakia na nguvu mingi wakubwa ya taifa ya Yuda, kwa sababu alisadiki ya kama wale walikuwa wakosefu ya uharibifu ya kabila yao. Mara nyingi Yeremia aliendа nyumbani kubwa ya mufalme Sedekias na alimushauria, lakini yeye alikataa kumutii na alimuchekelea. Lakini malipizi ilikuja mengi mbio-mbio. watu wa Yuda walimbakia kwa utumwa mujini Babilona ya Persia miaka makumi saba.

Yeremias walimufunga na walimufukuza mara nyingi kwa sababu alihubiri sauti ya kweli na uwezo mingi.

Yeremia aliacha unabii pahali aliandika ya kama itafika wakati, pahali Mungu atajenga taifa Izraeli mupya katika Mwokozi wetu Yesu Kristu, mwenye ataleta uzima mupya duniani.

Walimuua mu inchi Misri kwa sababu alihamakia wa ndugu wake, kwani walikana Mungu wa kweli. Kanisa yetu inashangilia ukumbusho yake mu tarehe siku ya kwanza Mwezi ya Tano.

## 4. Nabii Ezekieli.

Nabii Ezekieli aliishi mbele ya uharibifu ya ufalme wa Yuda, karibu ku mwaka 597, mbele ya uzalio ya Kristu. Aliendа na yeye mutumwa mujini Babilona ya Persia. pale alimwita Mungu pa cheo ya unabii. Aliona Mungu kwa ono moja kuikaa pa Kiti kubwa na alisikia hii ma neno: «Mwana wa watu, ninakutuma kwa wana wa Izraeli, kwa mataifa waasi walioniasi; wao na baba zao walinikosea, hata kufika leo. Nao wana hawana haya, nao ni wenye mioyo migumu; ninakutuma kwao; nawe utawaambia (maana wao ni nyumba ya kuasi), watajua hata hivi ya kama nabii amekuwa katikati yao. Nawe, mwana wa watu, usiwaogope, wala usiogope maneno yao, hata michongoma na miiba ikiwa pamoja nawe na unakaa katikati ya nge; usiogope maneno yao, wala usifazaike kwa nyuso zao hata wao ni nyumba ya kuasi» (Ezekieli 2, 3-6).

Yeye aliona, mbele ya miaka nyingi, uharibifu ya ufalme wa Yuda na utumwa ya taifa toka wakubwa ya Babilona. Sawa vile Yeremia, wakati ya utumwa mujini Babilona, alitumika na alihubiri toba mu taifa ya Yuda, hivi na Ezekieli hile wakati alitumika na alihubiri watumwa wa ndugu wake mujini Babilona ya Persia. Kitabu yake inashauria taifa wa Yuda kuvumilia kwa ajili ya mateso yao na, tena anawashauria ya kama hii mateso yao, itawasafisha kwa ajili ya zambi wao. Anahubiri ndani ya Kitabu yake kwa kutubu taifa lake na anawalaka ya kama watapowa na tena anawaambia ufikisho ya Bwana Yesu Kristu duniani.

Mungu alionyesha maono moja kwa nabii yake Ezekieli juu ya kumuonyesha tengenezo ya ufalme ya Yuda. Mungu alimupeleka mu kiwanja moja, pahali ilikuwa mifupa ya watu nyingi na alimusukuma kuhamuru mifupa yote kupata miili yao na kupata uzima yao. Na kweli hii jabo ilifanyikwa.

Tena Ezekieli alisema ya kama ufalme wa Kristu itakuwa pa fasi yote ya dunia.

Huyu Nabii taifa alimuua ku mwaka 570 mbele ya uzalio ya Kristu. Kanisa yetu inashangilia ukumbusho yake mu tarehe 23 Mwezi ya Saba.

Hapa chini tunaweka ono hile aliona Nabii Ezekieli:

Unabii wa Ezekieli (37, 1-14)

Mukono wa Bwana ulikuwa juu yangu, akanichukua inje kwa Roho ya Bwana, akaniweka chini katika bonde; likajaa na mifupa. Akanifanya kuizunguka pande zote; na tazama, ilikuwa mingi sana juu ya uso wa bonde; na tazama, ilikuwa mikavu sana. Akaniambia: Mwana wa watu, mifupa hii inaweza kuishi? Nikajibu: Ee Bwana Mungu, wewe unajua. Akaniambia tena: Tabiri juu ya mifupa hii uiambie: Ee ninyi mifupa mikavu, sikieni neno la Bwana. Bwana Mungu anasema hivi kwa mifupa hii: Tazameni, nitafanya pumuzi kuingia ndani yenu na mutaishi. Na nitaweka mishipa juu yenu na kuleta nyama juu yenu, na kuwafunika ninyi na ngozi, na kutia pumuzi ndani yenu, na mutaishi, na mutajua ya kama mimi ni Bwana. Basi nilitabiri sawasawa nilivyoagizwa; na wakati nilipotabiri, ilikuwa sauti, na tazama, tetemeko la inchi, mifupa ikakaribiana, mufupa kwa mufupa wake. Nikaangalia, na tazama, mishipa ilikuwa juu yao, nyama ikatokea, na ngozi iliifunika; lakini pumuzi haikuwa ndani yao. Halafu akaniambia: Tabiri kwa upepo, tabiri, mwana wa watu, ukauambie upepo: Bwana Mungu anasema hivi: Toka katika pepo ine, ee pumuzi, ukawapuzie hawa waliouawa, waishi. Basi nikatabiri sawasawa alivyoniagiza, pumuzi ikawaingia, wakaishi wakasimama juu ya miguu yao, jeshi kubwa sana. Halafu akaniambia: Mwana wa watu, mifupa hii ni nyumba nzima ya Israeli; tazama, wanasema: Mifupa yetu imekauka, na taraja yetu imepotea; tumekatiwa mbali kabisa. Kwa hivi tabiri, ukawaambie, Bwana Mungu anasema hivi: Tazameni, nitafungua makaburi yenu, na kuwapandisha ninyi toka makaburi yenu, ee ninyi watu wangu; na nitawaleta ninyi kwa inchi ya Israeli. Na mutajua ya kama mimi ni Bwanja, wakati nitakapokwisha kufungua makaburi yenu, na kuwapandisha ninyi toka makaburi yenu, Ee watu wangu. Na nitaweka roho yangu ndani yenu, na mutaishi, na nitawaweka ninyi katika inchi yenu wenyewe na mutajua ya kama mimi Bwana niliyasema, na kuyafanya Bwana anasema.

## 5. Nabii Danieli

Na Danieli ni katikati ya ma Nabii makubwa. Huyu alikuwa mukubwa ya inchi yake na alitumika sawa Nabii katikati ya wakubwa ya inchi. Mbele ya wafalme wa inchi Persia a; iwahubiri ya kama dini ya pagano ni wa wogo na aliwafundisha ya kama Mungu ni paka Moja na wa kweli.

Mafundisho na masomo ya unabii yake ni ndani ya Kitabu na jina yake. Huyu tena alibeba zawadi ya Mungu kufafanusha ma ndoto. Huyu tangu ujana kidogo alipelekwa nyumbani kubwa ya mfalme ya muji Babilona na pale alifata mafundisho ya kuachana na alibeba ma cheo ya hile inchi.

Alifafanusha ndoto moja ya mfalme Nebukadneza wa Pili. Mufalme aliona mu ndoto yake sanamu moja urefu na kichwa yake ilikuwa na zahabu, kilari na mikono yake ni na argind, miguu yake ilikuwa kipande moja na sabo na kipande ingine na matope. Mara moja alitelemuka jiwe moja toka kilima wa karibu na alivunja hile sanamu. Kisha hii jiwe ilifanyika kilima na alikamata inchi yote.

Nabii Danieli alifafanusha ndoto hivi: Kichwa wa zahabu ilikuwa ufalme ya Nebukadneza, hile kipande ya sanamu ilikuwa ya argind ilikuwa mamlaka ya taifa wa Persia, hile kipande ya samba ilikuwa mamlaka ya mfalme wa Grekia Aleksandros mkubwa na hile kipande ya sanamu iliyekuwa na sabo ilikuwa mamlaka ya ufalme wa Roma, iliyekuachana mu kipande ya mashariki na kipande ya magaribi. Hile jiwe ilikuwa Yesu Kristu, na ufalme wake ilizambalala mu dunia mzima. Na kweli hii yote ilifanyikwa.

Hile wakati walikuwa wakubwa taifa ya inchi Media, mufalme wao Dario alimupatia Danieli cheo juu ya kuangalia wakubwa wengine mu inchi yake. Hii sifa ilileta chuki kwa wakubwa wengine na waliwaza namna gani watamuua Danieli. Hawa walisema kwa mufalme Dario kutuma ma fasi ya inchi yake yote barua moja, na ataandika watu ya taifa yake haipaswe kuomba hata kintu moja hata toka Mungu, hata toka watu wengine, paka wataweza kintu kimoja paka toka mufalme wao. Lakini Danieli alifanya sala kwa Mungu mara tatu kila siku na aliomba kila kintu yeye alikuwa na lazima. Basi, hile wakati yeye aliomba kila kintu yake, ma adui wake walimubamba na walimusitake kwa mfalme. Basi, Dario alihamuru kumutupa ndani ya kisima moja, pahali walikuwa na ma simba. Lakini ma nyama makali hawakumuuzi Nabii Danieli, kwa sababu Malaika ya Mungu alimuchunga. Mufalme Dario alisikia hii muujiza, alimupoa Danieli na ndani ya hile kisima alituma ma adui wake. Tena aliandika na alituma amri yake watu wa taifa yote kumuabudu Mungu ya Danieli.

Nabii Danieli aliandika unabii juu ya ufikisho ya Bwana Yesu Kristu duniani. Aliita Kristu Mwana wa Mutu, kwani aliona Bwana Yesu sawa mutu katika ono moja wa ajabu. Tena alisema ya kama Kristu atasulubiwa kisha miaka 490. Alikufa muzee kabisa. Ukumbusho yake Kanisa yetu inashangilia mu tarehe 17 Mwezi ya kumi na mbili.

## 6. Nabii Elia

Nabii Elia alikuwa nabii moja katikati ya Manabii ya Izraeli na Mungu alimutuma kwa mufalme Akhaavi mwenye kibego juu ya kumuhukumu tabia kibaya yake na kwa sababu alifata dini ya upagano. Lakini, Akhaavi alizarau ma shauria ya Nabii na tena alimufokea ya kama atamuua. Nabii Elia alisema kwake: «Ninalaka hapa sasa, mbele ya Mungu, ya kama haitanyeshe nvula, wala ufalme wako itapata baridi mpaka mimi nitamuomba Mungu kusimamisha kipwa». Ya wakati miaka wa tatu haikuanguka hata tone moja ya nvula mu ufalme yote na taifa alianza kufa kwa kihu. Huyu mufalme mubaya alikuwa na bibi moja, jina yake Yezaveli, mwenye alikuwa kupita mubaya ya kwake na huyu bibi alimukokota kufata dini ya upagano. Wote wa wili waliogopa na walimutafuta Nabii Elia. Ku mwisho Elia, katika amri ya Mungu, alionekana kwa Akhaavi, mwenye , wakati alimuona, alisirika sana.

-Weye, basi, alimwambia, unafanya matendo mbaya mengi ndani ya ufalme wangu?

-Hapana mimi, alimujibu Nabii, lakini weye mumoja, kwani na weye na taifa yako muliacha Mungu wa kweli.

Wakati moja Elia alikuta mujini Sarepte ya inchi Finiki mwanamuke moja mbalaka na maskini, aliyeishi pamoja na mwana wake. Huyu mwanamuke alimupokelea na alimukaribisha nyumbani yake, hata na hii bunga kidogo na mafuta, ilikuwa nyumbani wake. Lakini ilifanyika muujiza na sala ya Nabii. Hivi hii bunga na mafuta hakuna namna kuishi mpaka hile siku ilinyesha nvula na inchi ilianza kuzala matunda. Nabii Elia alifanya tena na muujiza ingine nyumbani ya hule mwanamuke maskini. Alimufufusha mwana wake, mwenye aliisha kufa.

Nabii WElia alifanya matendo mengi wa ajabu na hivi anaitwa Mkubwa. Lakini Nabii alifanya na ingine muujiza pa kilima Karmilon mbele ya wafalme Akhaavi na bibi wake Yerzaveli juu ya kuwaonyesha ya kama dini ya wapagano ni ya wogo.

Aliomba kuchinja ngombe wa wili. Ngombe moja alimutoa kama sadaka kwa Mungu Nabii Elia na ngombe mwingine walimutoa  wapadri wa sanamu mbele ya mungu wao, jina lake Vaali. lakini waliichika mbele ya kama hawatawakisha moto. Moto itakuja hii wa pekee toka mbingu katika sala yao. Kama Vaali alikuwa mungu wa kweli, ilipaswa kuanguka moto toka mbingu katika ma sala ya wapadri wa sanamu. Hivi itawakisha moto ya sadaka wao. Kama, Mungu wa Elia alikuwa wa kweli, itaanguka moto toka mbingu pa sadaka ya Elia.

Hii sauti ya Nabii Elia iliipendezwa mu taifa  na walikamata mpango kufanya hivi.

Wapadri wa mungu Vaali, walichinja ngombe, walimuweka pa kuni na walianza kumuomba Vaali wote pamoja. lakini hata moto, wala jibu! Walicheza, walitembea pembeni ya fasi ya sadaka, lakini hakuna kintu, kwani huyu mungu hasikukuwe wa kweli.

Hile wakati Elia aliita taifa kukaribia ku fasi ya sadaka ya Mungu wa kweli. Aliweka nyama na ma kuni na alihamuru kutupa pembeni maji mingi. Maji ilizuguluka pembeni juu hapana kuwaza mutu fulaniya kama ilikuwa moto ya zamani.

Ee Bwana, alisema Elia, Wewe ni Mungu wa kweli wa pekee ya Abrahamu, Isaaka na Yakobo. Ninakuomba unisikie na unitume moto toka mbingu juu ya kufanya sadaka na kufamia watu wote leo ya kama Weye uko Mungu wa kweli na mimi ni mutumishi Wako na hii matendo yote inafanyikwa katika amri Yako.

Mbele kusema ma sauti yake wa mwisho Elia, ilikuja moto nguvu toka mbingu na alilungua  tena na ma jiwe na kuni na yoyote vitu.

Wakati aliona taifa hii muujiza, alisadiki kwa Mungu wa kweli. Wakati Elia aliona ya kama walitubu, aliomba kwa Mungu na alinyesha nvula. Huyu taifa aliyeona muujia hii alitukuza Mungu.

Mungu alimustahili Elia kupanda mbinguni, bila kupima lufu. Upandisho yake ilifanyika karibu ya mtoni Yorodani. Hile wakati alipanda mbinguni, alitupa chini ngozi yake kwa mwanafunzi wake, Nabii Eliseyo na huyu kisha alifanya miujiza ya kuachana na hii ngozi ya Nabii Elia.

Kanisa yetu anamushangilia mu tarehe 20 Mwezi ya Saba.

## Ma Nabii wadogo

### 1. Hosea.

Huyu Nabii aliishi ndani ya ufalme ya Izraeli ku milele wa mnane, mbele ya uzalio ya Kristu. Alikuwa mutu wa hekima, kwani alijua nzuri Hadisi ya Izraeli na Kitabu yake ni muzuri sana.

Katika amri ya Mungu aliowa mwanamuke jina lake Gomeri na alizala watoto wa tatu. Nabii alitembelea ma fasi takatifu ya inchi yake na kabisa wakati ilikuwa ma shangilio yao na pale mbele ya watu nyingi aliwahubiri mapenzi na fundisho ya Mungu.

Namna gani Hosea Mungu alimwita kwa hii cheo yake hatujue. Fundisho kubwa yake ilikuwa hali wa dini mu taifa yake. Hosea alisirika kwa sababu taifa lake anaabudu ma sanamu na anahubiri kupingana ya upagano katika nguvu ya Mungu. Aliandika unabii ya kama Mwokozi atazaliwa toka kizazi ya Mfalme Daudi. Ndani ya unabii wake tunapata fundisho nzuri, ya kama Mungu anataka mapendo toka taifa lake na hapana sadaka. Tazama unabii moja:

**«.. . Ninataka mapendo na hapana sadaka. »**

«Kujeni turudi kwa Bwana; kwa maana amepasua naye atatuponyesha; amepiga naye atatufungia kitambaa. Nyuma ya siku mbili atatufufua, siku ya tatu atatusimamisha nasi tutaishi mbele yake. Kisha tutajua kama tukiendelea kujua Bwana; kutokea kwake ni hakika kama asubui; naye atakua kwetu kama mvua, kama mvua ya myuma inayotia maji juu ya inchi. ee Efuraimu, nitakufanyia nini? Ee Yuda, nitakufanyia nini? Kwa kuwa wema wako ni kama wingu ; a asubui, na kama umande unaoondoka mapema. Kwa sababu hii nimewakatakata kwa manabii, nimewaua kwa masemo ya kinywa changu; na hukumu zako ni kama nuru inayotoka. Kwa maana ninataka rehema, hapana zabihu, na kujua nuru Mungu kuliko sadaka za kuteketezwa» (Hosea 6, 1-6).

## 2. Amosi

Nabii Amosi aliishi ku milele wa mnane mbele ya uzalio ya Kristu. Mukini yake ilikuwa Thekoa, muji kidogo ndani ya ufalme wa Yuda. Huyu mu uzima yake alikuwa muchungaji. Tena alikuwa na mulimaji. Lakini alikuwa na hekima na mwangaza mu akili yake. Mungu alimwita mu cheo yake juu ya kuhubiri watu toba na kurudia mu dini ya Mungu wa kweli.

Mungu, ku mwanzo ya kazi ya unabii yake, alimuonyesha aktika maona ya kama itaharabika ufalme wa Yuda. Ndani ya ono anaonekana panjo moja na hii anakula mayani yote ya inchi wa Yuda. Nabii aliogopa sana na mwenye kujaza roho yake na mapendo mu taifa, alimuomba Mungu aokoe taifa lake. Na kweli uharibifu hasikufike. Lakini taifa hasitobe. Ono wa pili na watu aliona Nabii na yeye alimuomba Mungu na kuhubiri kwa taifa, lakini taifa wa Yuda anabakia asiye na toba na vile uharibifu inakuja.

Nabii Amosi aliandika unabii juu ya Usulumbio ya Bwana Yesu, ya kama ilifanyika giza, wakati Yeye alikuwa pa Msalaba na ya kama atafufuka siku wa tatu.

Tazama ma sauti ya unabii wake: «Na itakuwa siku ile, Bwana Mungu anasema, nitashusha jua kwa saa sita azuhuri, na nitatia giza katika inchi kwa siku ya nuru. na nitageuza karamu zenu kuwa maombolezo, na nyimbo zenu kuwa vilio, na nitaleta gunia kwa viuno vyote, na upaa kwa vichwa vyote; na nitayafanya kama maombolezo kwa mwana aliye pekee, na mwisho wake kama siku ya uchungu» (Amosi 8, 9-10).

## 3. Mika

Aliishi ku milele wa mnane, mbele ya uzalio ya Kristu. Fundisho yake inaiongoza kupingana ya watu wakubwa ya taifa lake. Na huyu alikuwa muchungaji. Alipenda sana wale watu walikuwa chini ndani ya taifa. Ndani ya manabii yake aliandika ya kama Kristu atazaliwa mujini Betelehemu na Kristu alikuwa mbele ya milele.

Pa fasi moja ya fundisho yake aliandika juu ya Yerusalema mupya, hile ataleta Bwana Yesu Kristu. Tazama hii unabii wake: «Lakini katika siku za mwisho itakuwa, mulima wa nyumba ya Bwana utawekwa imara juu ya milima, na utapandishwa juu ya vilima; na mataifa watamukimbilia. Na makabila mengi watakwenda na kusema: Kujeni, twende kwa kilima cha Bwana, na kwa nyumba na Mungu wa Yakobo, naye atafundisha njia zake, nasi tutakwenda kwa mapito yake; kwa maana katika Sayuni sheria itatoka, na neno la Bwana toka Yerusalema. Naye atahukumu kati ya mataifa mengi, na atahamakia makabila ya ya nguvu ya mbali, nao watafua

panga zao kuwa majembe, na mikuki yao kuwa miundu; taifa halitanyanyua upanga juu ya taifa, wala hawatajifundisha kupiga vita tena. Lakini watakaa, kila mutu chini ya muzabibu wake, na chini ya mutini wake; wala hapana mwenye kuwaogopesha, kwa maana kinywa cha Bwana wa majeshi kimesema hivi» (Mika 4, 1-4).

## 4. Yoeli

Nabii Yoeli alikuwa mwana wa Vathuili na aliishi ku milele wa tisa, mbele ya uzalio ya Kristu. Manabii yake wanasema mambo yote ya muji Yerusalema, Hekalu na hile malako Mungu alisema mu taifa wa Yuda. Yoeli alikuwa mutu mwenye hekima. Ndani ya fundisho yake anaandika ya kama uabudu wa ndani ya kupita kubwa ya hile uabudu wa inje. Anataabu kwa ajili ya mateso ya taifa na anasadiki ya kama paka Mungu anaweza kuwaokoa.

Yeye aliandika unabii juu ya ufikisho ya Roho Mtakatifu, Ufikisho wa mbili ya Bwana yesu na Uhukumu wa mwisho.

Tazama somo ya unabii juu ya ufikisho ya Roho Mtakatifu: «Na itakuwa nyuma ya maneno haya, nitamwanga Roho yangu juu ya watu wote; na wana wenu na binti zenu watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, vijana wenu wataona maono; na vilevile juu ya watumishi wangu, wanaume na wanawake, nitamwanga Roho yangu katika siku zile. Na nitaonyesha maajabu katika mbingu na katika dunia, damu na moto na nguzo za moshi. Jua litageuka kuwa giza, na mwezi kuwa damu mbele ya kutimia kwake ile siku kubwa ya Bwana, yenye kuogopesha. Na itakuwa kila mutu atakayeomba kwa jina la Bwana, ataokolewa. Kwani katika kilima Sayuni na katika Yerusalema watakuwa wenye kuokolewa, kama Bwana alivyosema, na katika baki wale Bwana anaowaita» (Yoeli 2, 28-32.

## 5. Obadia.

Aliishi ku milele wa tisa, mbele ya uzalio ya Kristu. Paka jina lake sisi tunajua. Toka Kitabu wake tunasikia ya kama alikuwa toka ufalme wa Yuda. Anatufindisha katika manabii wake ya kama Mungu ni mwenye haki na analipa kila mtu, katika matendo yake. Aliandika unabii ya kama ufalme wa Kristu itakuwa bila mwisho. Tazam unabii: «Kwa maana siku ya Bwana ni karibu juu ya mataifa yote; sawasawa ulivyofanya itakufanyiwa; tendo lako litarudi juu ya kichwa chako mwenyewe» (Mustari 15).

## 6. Yona.

Huyu aliishi ku milele wa mnane, mbele ya uzalio ya Kristu. Mungu alimutuma kuhubiri toba mu taifa ya muji Ninawe ya inchi Asiria, lakini alikataa kutii. Alipanda pa chombo moja na alikimbia. Chombo iliteswa kwa ajili ya tufani ya bahari na Yona watu walimutupa baharini sawa mukosefu, kwa sababu alikataa kufata amri ya Mungu. Samaki moja mnene alimukula Yona na kisha ma siku tatu, alimutosha katika sala yake. Hii jabo ilituonyesha maziko na ufufuo wa siku tatu ya Bwana Yesu Kristu.

Kisha Yona alienda mujini Ninawe na alihubiri toba kwa watu ya hile muji.

**Sala ya Yona ndani ya tumbo ya samaki**

«Kwa maana umenitupa vilindini, katika moyo wa bahari, Garika imenizunguka; mawimbi yako yote na garika zako zote zimepita juu yangu. Nikasema: Nimetupwa mbali na macho yako, hata hivi nitatazama tena kwa hekalu lako takatifu. Maji yamenizunguka hata nafsi; kinindi kimenizunguka; majani bule yamefunga kichwa changu. Nikashuka hata chini ya milima;

Inchi na mafungo yake yamenizunguka milele; Hata hivi umepandisha uzima wangu toka kaburi, ee Bwana Mungu wangu. Wakati nafsi yangu ilipozimika ndani yangu, nikakumbuka Bwana, na maombi yangu yamefika kwako katika hekalu lako takatifu. Wanaacha rehema zao. lakini nitatoa zabihu kwako kwa sauti ya kushukuru; Nitalipa kiapo nilichoapa; Wokovu unatoka kwa Bwana. Na Bwana alisema na samaki, akatapika Yona juu ya pwani» Yona 2, 3-10).

## 7. Nahumu

Nabii Nahumu alizaliwa mu inchi wa Yudea, ku milele wa saba mbele ya uzalio ya Kristu. Yeye alipenda sana inchi yake na alihubiri na mapendo mingi juu ya kuichunga. Alihubiri unabii juu ya uharibifu ya Ninawe na inchi ya Asiria.

Tena alisema ya kama Evangelio italeta amani na furaha mu duinia muzima.

## 8. Habakuki.

Nabii Habakuki aliishi ku mwaka 600, mbele ya uzalio ya Kristu. Miaka wa kwanza wake aliishi na amani na wa heri ndani ya ufalme wa Yuda. Yeye alikuwa mwenye hekima na aliisha kusoma makitabu ya ma Nabii wenye waliishi zamani na ku mukongo yake. Yeye alisema juu ya uharibifu ya ufalme wa Yuda na uharibifu ya inchi wa Babilona. Habakuki alihubiri ya kama Mungu ni Rabi mkubwa ya ulimwengu muzima, wa milele, asiye na kufa na mkubwa ya Hadisi ya dunia mzima. Tena alifundisha ya kama «mutu mwenye haki ataokolewa toka imani».
**Tazama Unabii yake moja:** «Tazama nafsi yake imejivuna, haina haki ndani yake, lakini mwenye haki ataishi kwa imani yake. Ndiyo, zaidi ya haya, mvinyo ni muchuruzi mwenye hila, mutu wa kiburi, asiyekaa nyumbani mwake; anaongeza tamaa yake kama kuzimu, naye ni kama mauti, wala hawezi kushibishwa, lakini anakusanya kwake mataifa yote. » (Habakuki 2, 4-6).

## 9. Zefania.

Nabii Zefania alikuwa mwana wa Khusi, mutu moja aliyeishi mu milele wa saba, mbele ya uzalio ya Kristu. Yeye anahukumu dini ya upagano na anita taifa arudie kwa kumuabudu Mungu wa kweli. Anamufundisha taifa ya kama Mungu anamupenda na anahubiri ya kama wokovu ya dunia toka zambi yake itakuja toka Bwana Yesu Kristu Mwokozi wetu.
**Unabii moja: Utukufu ya Sayuni.**

«Imba, ee binti ya Sayuni; paza sauti, ee Israeli, furahi na kushangilia kwa moyo wote, ee binti ya Yerusalema. Bwana ameondosha hukumu zako, ametupa inje adui yako; mufalme wa Israeli, hata Bwana, ni katikati yako; hutaogopa ubaya tena. katika siku ile itaambiwa kwa Yerusalema: Usiogope, ee Sayuni, mikono yako isilejee. Bwana, Mungu wako ni katikati yako mwenye uwezo kuokoa; atafurahi juu yako kwa furaha, atapumzika katika mapendo yake, atafurahi juu yako na kuimba. Nitawaokota wanaohuzunishwa kwa kusanyiko la dini, walio wa kwako; muzigo juu yake ulikuwa laumu kwao» (3, 14-18).

## 10. Hagai.

Nabii Hagai aliishi ku milele wa sita, mbele ya uzalio ya Kristu. Alirudia toka Utumwa ya inchi wa Persia (muji Babilona) na pamoja na nabii Zekaria alishauria taifa wa Yuda, hile wakati ya mfalme wa Persia Dairo wa Istaspus, juu ya kuendelea majengo ya Hekalu, kwa sababu majengo iliisha kusimama kwa ajili ya nvita ya taifa wa Samaria.

## 11. Zekaria.

Nabii Zekaria alikuwa padri. kazi yake ilikuwa kwa kumupatia nguvu taifa na alimushauria kufata imani ya Mungu. Huyu alisema ma jabo mengi ya uzima ya Bwana yesu Kristu. Tena alisema juu ya Kuingia Kristu mujini Yerusalema sawa mufalme wa amani; juu ya utoaji ya mutoaji Yuda, juu ya ma feza makumi tatu na ya kama Kristu atatoa sadaka pa Msalaba wake maungo Yake.

**Unabii juu ya Kungia kwake mu Yerusalema:**

«Furahi sana, ee binti ya sayuni; piga kelele, ee binti ya Yerusalema; tazama mufalme wako anakuja kwako; mwenye haki, na akiwa na wokovu, mwenye unyenyekevu na anapanda kipunda, hata mwana wa punda. (9, 9)

**Unabii juu ya feza makumi tatu:**

«Nikawaambia: Kama mukipendezwa, munipe mushahara wangu; sivyo, acheni. Basi, walipima vipande vya feza makumi tatu kwa mushahara wangu.. . » (11, 12).

## 12. Malaki.

Nabii malaki ni nabii wa mwisho ya manabii wote ya Agano la Kale. Kisha yake hasikuonekana Nabii mwingine, paka Nabii Yoane Mutangulzi na Mbatizaji ya Kristu. Huyu Malaki alisema juu ya ufikisho ya Yoane Mutangulizi. Tena alihubiri taifa ya Yuda ya kama Mungu hasitachelewa kutuma Yesu Kristu duniani. Alisema tena ya kama sadaka mupya itakombola ma sadaka ingine ya taifa. Hii sadaka itakuwa Usulumbio ya kristu na Shukrani Takatifu (Komonyo takatifu).

**Unabii juu ya ufikisho ya Nabii Yoane:**

«Tazameni, nitatuma mujumba wangu, naye atatayarisha njia mbele yangu: Na Bwana munayemutafuta atakuja mbio hekaluni mwake; na mujumbe wa agano munayemupenda, tazameni, anakuja, Bwana wa majeshi anasema. Lakini nani atakayehimidi kwa siku ya kuja kwake? Na nani atakayesimama wakati atakapoonekana? Kwa maana yeye ni kama moto wa mwenye kusafisha, na kama sabuni ya mwenye kufua nguo; naye atakaa kama mwenye kusafisha na kutakasa feza, naye atatakasa wana wa Lawi, na atawasafisha kama zahabu na feza, nao watatoa kwa Bwana matoleo kwa haki. Kwa waakti ule toleo la Yuda na Yerusalema litapendeza Bwana, kama kwa siku za kale, na kama kwa miaka ya zamani» (Malaki 3, 1-4).

## Mafundisho ya Manabii juu ya Mungu na uzima ubikira

Fundisho ya Manabii wote iko na katikati sauti ya Mungu. Mungu ni Mkubwa kabisa ya ulimwengu muzima. Nguvu Yake inafika ma fasi yote, kwa mbingu, kwa Hadeze, na chini sana ya bahari. Mungu anafanya tetemeko, giza ya jua, anatuma pepo wa moto, anasimamisha nvula, analeta njala na ugonjwa, wakati watu wanaepuka toka amri wake. Dunbia muzima inatetemeka na ndani ya dadika moja inapotea, wakati Mungu atasirika. Lakini kabisa Mungu ni mwenye haki.

Mungu wa Manabii hana paka Mungu watu wa Izraeli, sawa vile hawa walisadiki. Huyu ni Mungu wa ulimwengu na anatembesha vitu vyote vya dunia. Bila mapenzi Yake, haifanyika kintu. Mungu Mwenyezi na mwenye ulimwengu ni ma fasi yote.

Huyu ni Mtakatifu kabisa. Huyu aliweka ma amri ya uzima ubikira na takatifu. Muvunjo ya ma sheria takatifu, katika ma sauti ya Manabii, inaleta mara moja malipizo. tena Manabii wanafundisha ya kama sheria ya uzima takatifu ni ndani ya moyo ya kila mtu. Kwa hivi Manabii yote karibu wanahukumu zambi ya mwili ya wale watu mu wakati wao na wanasema ya kama itawafata uharibifu, na hii itakuja kwa ajili ya zambi yao.

Katika mafundisho ya Manabii Wakubwa ni wakosefu kama ma taifa wao wanaepuka toka Mungu.

Fundisho kuliko kubwa yao ni ya kama , hawa Manabii, waliishi miaka mengi mnbele ya uzalio ya Kristu, lakini walisema juu ya ufikisho Yake na ya kama Huyu ni atakuwa Mwokozi ya

dunia muzima. Hata nguvu na safi walisema juu ya matendo na jabo yote ya Bwana Yesu, na iko namna kuzania mtu moja ya kama, waliona na kisha waliandika hii matendo yote.

Mafundisho yao ni karibu pa fasi moja pamoja na mafundisho ya Agano Jipya, kwani mafundisho yao juu ya Mungu na uzima takatifu ni umoja karibu ya mafundisho ya Agano Jipya na hivi sisi tunasadiki ya kama hawa wanaume Mungu aliwatuma duniani.

Huyu Bwana Yesu Kristu na Mwokozi wetu, Manabii waliona matendo na uzima yake mbele ya uzalio yake. Huyu Mwokozi wetu tutamufunda mu Kitabu Agano Jipya.

## NENO KIFUPI

Tangu hile wakati Mungu Muumba wetu alifukuza toka Paradizo wazazi wa kwanza, kwa ajili ya kukanyanga amri Yake, tangu hile wakati, alikamata mpango kutuma sawa Mwokozi na Mukombozi ya dunia Mwana wake wa pekee na Mungu wetu, Bwana wetu Yesu Kristu.

Hii mpango Yake aliijulisha na kwa wazazi wa kwanza. Kisha wakati ingine aliisema mara infgine katika hile sauti alisema Noa kwa watoto wake.

Tena Mungu aliita Wapatriarkhes Abrahamu, Isaaka na Yakobo na alisema kwao ya kama toka kizazi wao atazaliwa Mwokozi. Hii sauti alisema na Yakobo, ya kama toka kizazi ya mwana wake wa inne, jina yake Yuda, atazaliwa Mwokozi, na huyu atakuwa kitumaini ya ma inchi yote.

Tena tunaona ya kama Mungu alichakula taifa wa Yuda juu ya kutengeneza ufikisho ya Mwokozi duniani na hivi tulijua Hadisi ya hule taifa, na huyu kisha utumwa wake mu Msiri, alipata, katika mapenzi ya Mungu, mkubwa Nabii Musa juu ya kupata na uhuru wake.

Musa aliongoza taifa ya Yuda katikati ya jangwa ku inchi ya Palestina. Mungu alifanya miujiza mengi katika mutumishi wake Musa juu ya kusaidia taifa Lake katikati ya jangwa.

Mara mengi aliwalipiza kwa ajili walimusahau Mungu Baba wao, lakini mara ingine aliwasamehe na aliwalinzi, katika toba yao. Mu jangwa aliwapatia Sheria na aliwaambia kuichunga hii Sheria mu uzima wao.

Tena alituma kwao Waamuzi na wafalme, na katikati yao Mfalme na Nabii Daudi, mwenye alisema unabii ndani ya ma Zaburi wake juu ya ufikisho ya Mwokozi Yesu Kristu na kabisa toka kizazi yake.

Tena tunafunda mifano mengi ya mbalimbali ya imani na kabisa faida gani inaleta imani nguvu mbele ya Mungu.

Katika utume ya Manabii ilikuja duniani tangazo ya kama atakuja Mwokozi. Na Mwokozi alikuja ku mwaka 750 toka majengo ya muji Roma, mu wakati mubaya, kwa sababu ma dini ya ma pagano waliisha kuanguka chini sana mu moyo ya watu, kwa sababu hawakuweze kusaidia mutu kuokolewa; lakini na dini wa kweli hile wakati, nikusema dini ya Wayuda iliisha kuharabika kwa ajili ya udanganyifu na majivuno ya ma Kundi ya Wafarisayo na Wanandishi-Sheria na hivi dini yao ilikuwa paka ya kuchunga ma alama, bila faida ndani ya roho ya watu. Vile dunia muzima alipindula ma macho yake kwa Mungu Mwokozi, kwani Yeye ilikuwa namna kumuokoa toka mateso ya zambi yake.

**UTUKUFU KWA UTATU MUTAKATIFU**
**MONASTERI YA MTAKATIFU GRIGORIO**
**KILIMA TAKATIFU**
**GREKIA**
**2000**

